USAWIRI WA MASUALA YA KIJINSIA KATIKA LUGHA YA MASHAIRI: MIFANO KUTOKA MASHAIRI YA BONGO FLEVA TANZANIA

AMBARAK IBRAHIM SALEH KHALIFA

TASINIFU YA M.A KISWAHILI

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2013

USAWIRI WA MASUALA YA KIJINSIA KATIKA LUGHA YA MASHAIRI: MIFANO KUTOKA MASHAIRI YA BONGO FLEVA TANZANIA

AMBARAK IBRAHIM SALEH KHALIFA

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUKAMILISHA MASHARTI YA DIGRII YA M.A KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2013

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasinifu hii iitwayo: **Usawiri wa masuala ya Kijinsia katika Lugha ya mashairi: Mifano kutoka Mashairi ya Bongo Fleva**, na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya M.A. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sheikh, Professa, Dkt. T.S.Y.SENGO

(MSIMAMIZI)

Tarehe ----------

IKIRARI

NA

HAKIMILIKI

Mimi, **Ambarak Ibrahim Salehe Khalifa**, nathibitisha kuwaTasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digirii yoyote.

Sahihi.....

Haki ya kunakili tasinifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, Sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali ya kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya Tasinifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

SHUKURANI

Kwa hakika si kazi rahisi kuwataja na kuwashukuru kwa majina wote waliochangia kukamilika kwa utafiti huu. Hata hivyo, napenda kutumia fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamewezesha kukamilika kwa utafiti huu. Wafuatao wanastahili shukurani za kipekee.

Kwanza, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, aliyenijaalia afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Sheikh, Professa, Dkt. T.S.Y.Sengo kwa msaada wake usio na kikomo uliowezesha kukamilika kwa utafiti huu. Kwa hakika alijitoa sana katika kuniongoza, kunishauri, kunikosoa na kunielekeza katika hatua mbalimbali za utafiti wangu huu na hivyo kunilazimu kutumia muda mwingi kutafakari na kufanyia kazi maelekezo yake yaliyosaidia kukamilika kwa utafiti huu. Nakushukuru sana Mzee Sengo na nakutakia kila la kheri katika maisha yako wewe binafsi pamoja na familia yako.

Tatu, natoa shukurani zangu za dhati kwa mfadhili wangu wa masomo ambaye ni Serikali ya Watu wa Libya kwa kujitoa, na kuniwezesha kwa kunilipia gharama za masomo yangu ya uzamivu na gharama za kujikimu katika kipindi chote cha masomo yangu.

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa mzazi wangu **Ibrahimu Salehe Khalifa** na marafiki zangu wote ambao kwa hakika wamejitoa kwa hali na mali katika kufanikisha malengo yangu ya kitaaluma ambayo yamenifikisha hatua hii ya kutunukiwa **Shahada ya Uzamili** katika Kiswahili.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza masuala ya Kijinsia katika Lugha ya Mashairi: Mifano kutoka Mashairi ya Bongo fleva. Lengo hili limeweza kufanikiwa kutokana na kukamilika kwa madhumuni mahususi yaliyohusu, kubainisha tamathali za semi katika mashairi ya bongo fleva, kuonesha jinsi tamathali hizo zinavyosawiri mahusiano ya kijinsia, kubainisha nafasi ya mwanamke na mwanaume kama inavyosawiriwa na tamathali za usemi za mashairi ya bongo fleva na kuainisha tofauti baina ya wasanii wa kike na kiume katika kusawiri masuala ya kijinsia. Mapitio ya kazi tangulizi mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti yamepitiwa kwa kina kwa kuongozwa na nadharia za Simiotiki, Ufeministi na Umarx. Kwa upande wa uchambuaji, uchakataji na usanifishaji wa data, utafiti umetumia mbinu za ushiriki, usaili, hojaji na upitiaji wa nyaraka katika kukusanya data. Mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, lugha ya mashairi ya bongo fleva inasawiri vilivyo masuala kijinsia ambapo wote mwanaume na mwanamke pamoja na sifa zao zinaelezwa katika mashairi hayo. Matokeo ya utafiti yanaendelea kuonesha kwamba, mwanamke anasawiriwa kama mama, mlezi, jasiri na shujaa, mshauri na mchapakazi katika jamii. Vile vile, anasawiriwa kama Malaya, mvivu wa kufikiri na kiumbe rahisi kudanganyika. Mwanaume kwa upande wake anasawiriwa kama kiongozi wa nyumba, kiumbe mwenye uwezo mkubwa wa kufikiri, baba jasiri na shujaa. Vile vile, anasawiriwa kama mlevi, Malaya, mtelekeza watoto, kiumbe mwenye tama na asiyeridhika. Mwisho ni hitimishi, muhtasari na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

YALIYOMO

Uthibitisho..... ii

Ikirari na Hakimiliki iii

Shukurani iv

Tabaruku v

Ikisiri vi

Yaliyomo..... vii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1

1.0 MADA YA UTAFITI 1

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti..... 1

1.2 Tatizo la utafiti..... 3

1.3 Malengo ya Utafiti 4

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti 4

1.3.2 Madhumuni Mahsusi 4

1.4 Maswali ya utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 5

1.5.1 Mipaka ya Utafiti 5

1.6 Vikwazo ya Utafiti..... 6

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI 7

2.1 Utangulizi..... 7

2.1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Kuu..... 7

2.1.2 Tamathali za Semi..... 7

2.1.3 Tashibiha..... 8

2.1.4 Tashihisi 8

2.1.5 Taashira 9

2.1.6 Ishara 9

2.1.7 Taswira 9

2.1.8 Sitiari 10

2.2 Umuhimu wa Istilahi Tajwa Katika Kazi za Fasihi na Utafiti Wetu 11

2.3 Tafiti Tangulizi Katika Ushairi wa Bongo Fleva 12

2.4 Hitimishi 16

SURA YA TATU: NADHARIA YA UTAFITI NA UTEUZI 17

3.1 Mwega wa Kinadharia 17

3.2 Nadharia ya Umarx 17

3.2 Nadharia ya Simiotoki 19

3.3 Nadharia ya Ufeminist 20

3.4 Hitimishi 22

SURA YA NNE: MBINU ZA UTAFITI 23

4.1 Njia za Kufanyia utafiti 23

4.2 Usanifu wa Utafiti 23

4.3 Eneo la Utafiti 24

4.3.1 Kundi lengwa 24

4.4 Usampulishaji na Sampuli 24

4.4.1 Usampulishaji 24

4.4.2 Sampuli 25

4.4.2.1 Uteuzi wa Sampuli 25

4.4.2.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu 26

4.4.2.3 Uteuzi Nasibu..... 26

4.5 Ukusanyaji wa Data 27

4.5.1 Mbinu za Utafiti 27

4.5.1.1 Mbinu ya Usaili..... 27

4.5.1.2 Usaili Maalumu Uliowazi 28

4.5.1.3 Mbinu ya Majadiliano ya Kundi Lengwa 28

4.5.1.4 Mbinu ya Maktaba 29

4.6 Zana za Kukusanyia Data 29

4.8 Uhalali na Kuaminika kwa Mbinu za Utafiti 32

4.8.1 Uhalali wa Mbinu za Utafiti 32

4.8.2 Kuaminika kwa Data..... 32

4.9 Maadili ya Utafiti 32

4.10 Hitimishi 33

SURA YA TANO: UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA 34

5.1 Utangulizi..... 34

5.1.1 Masuala ya Kijinsia Katika Mashairi ya Bondo Fleva 34

5.1.2 Sifa ya Mwanamke Dhidi ya Mwanaume..... 34

5.1.3 Mwanamke Kiumbe Anayedanganywa Kirahisi 40

5.1.4 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe..... 45

5.1.5 Sifa na Mapambo kwa Mwanamke 49

5.1.6 Mwanaume Kupendwa na Mwanamke..... 54

5.1.7 Wanawake na Mapenzi ya Pesa..... 56

5.1.8 Mwanamke Mlezi wa Jamii/Familia 58

5.1.9 Mama Kiumbe Shujaa na Jasiri 62

5.1.10 Mwanamke kama Mshauri katika jamii 64

5.1.11 Mwanaume kama Kiumbe Msaliti wa Jamii 66

5.2 Kufanana Kutofautiana kwa Wasanii wa Kike na Kiume katika Kusawiri Masuala ya Kijinsia 68

5.3 Mchango wa Tamathali za Usemi katika Kusukuma Mbele Masuala ya Kijinsia 71

5.4 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti 74

5.5 Hitimishi 77

SURA YA SITA: MUHUTASARI, HITIMISHI, NA MAPENDEKEZO 78

6.1 Utangulizi 78

6.2 Muhtasari 78

6.3 Hitimishi 80

6.4 Mapendekezo 82

MAREJELEO 84

VIAMBATISHI 89

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 MADA YA UTAFITI

Mada ya utafiti huu ni **Usawiri wa Masuala ya Kijinsia katika Lugha ya Mashairi: Mifano kutoka Mashairi ya Bongo Fleva Tanzani.** Mada hii ya utafiti iliteuliwa kutokana na pengo la kiutafiti linalodhihirika katika kazi tangulizi tulizopitia. Kazi hizo kwa kiasi kikubwa zimegusia tu masuala ya lugha ya ushairi na ujinsia na hivyo kupwaya kwa maana ya kukosa maelezo ya kina juu ya masuala hayo. Utafiti huu ulifanywa ili kupata maelezo ya kina juu ya usawiri wa masuala ya kijinsia katika mashairi ya bongo fleva na kisha kuziba pengo hili la kiutafiti.

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo (Mulokozi, 1994). Kwa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi tunaweza kubadili mielekeo, mitazamo, tamaduni, imani, mila na desturi za jamii husika katika muktadha na wakati mahususi. Vile vile, fasihi simulizi inaweza kutumiwa kuzuia au kucheleweshа maendeleo na mapinduzi. Fasihi simulizi inasaidia kujifunza utamaduni wa umma; kuelewa msimamo, itikadi na mahitaji yao, na kuwasaidia kuitumia fasihi yao kuendeleza mapambano dhidi ya mazingira yao. Hivyo ni wazi kuwa fasihi simulizi huweza kuibua masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii na kuleta athari kwa jamii kwa haraka zaidi (Mulokozi, 1983).

Fasihi simulizi ni utanzu wa fasihi ambao una tanzu nyingi. Moja wapo ya tanzu za fasihi simulizi ni ushairi. Ushairi ni utungo unaotumia lugha ya mkato yenye mnato

na mvuto katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii (Mulokozi na Kahigi, 1973). Ushairi una tanzu nyingi ambapo mashairi ya bongo fleva ni moja ya utanzu wa ushairi (Omari, 2009). Bongo fleva ni utanzu ambao umeibuka miaka ya 1980 na umeshamiri na kupendwa sana na vijana wa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla. Kwa kutumia nyimbo hizi vijana wanaelezea hisia zao, matamanio yao, matarajio yao, kukata tama kwao na uzoefu wao katika jamii yao (Senkoro, 2003).

Utafiti huu unachunguza usawiri wa masuala ya kijinsia katika lugha ya mashairi kwa kutumia mifano kutoka mashairi ya bongo fleva. Kimsingi, lugha ina vipengele mbalimbali ambavyo hutumiwa na wasanii wa kazi za sanaa katika kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, si kazi rahisi kutumia utafiti huu kuchunguza lugha yote kwa ujumla katika mashairi ya bongo fleva. Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza kipengele cha tamathali za semi tu. Hivyo basi, kwa kutumia utafiti huu tumeweza kuchunguza kipengele hiki na jinsi kinavyosawiri suala la ujinsia katika mashairi ya bongo fleva. Jilala (2008) anadai kuwa, kazi za wasanii hawa zimeonesha kuwa na utajiri mkubwa wa utumizi wa sitiari ambazo huzipa kazi hizo uzuri, ujumi na thamani ya kisanaa. Wasanii wa mashairi ya muziki wa kizazi kipya hutumia sitiari kisanii kuibua na kumsawari mwanamke na nafasi yake katika jamii. Vile vile, sitiari hizo huakisi muelekeo na utamaduni wa jamii kuhusu mwanamke. Sitiari humchora mwanamke katika taswira hasi na katika muktadha mwingine mwanamke huchorwa katika taswira chanya. Hivyo basi kutokana na utafiti uliofanywa na jilala (2008) tunaona kuwa kuna haja ya kuchunguza jinsi tamathali za semi katika mashairi ya bongo fleva zinavyosawiri masuala ya kijinsia kwa kina ambalo ndilo lengo kuu la utafiti huu.

1.2 Tatizo la utafiti

Tafiti mbalimbali zimefanywa katika mashairi ya bongo fleva na wanataaluma mbalimbali kama vile, Senkoro (2003); Jilala (2008) na Omari (2009). Watafiti wote hawa wamejikita katika kuchunguza masuala ya kifani na kimaudhui katika mashairi ya bongo fleva na hatimaye wote wanaonesha kuwa washairi wa bongo fleva huitumia lugha kisanii ili kujenga maudhui kwa lengo la kukosoa, kuelimisha, kuadibu, kutunza amali za jamii na hata kuelezea hisia zao na matamanio yao katika jamii. Hata hivyo, kulingana na uelewa wangu hakuna utafiti uliokwishafanywa kuhusu usawiri wa masuala ya kijinsia katika lugha ya mashairi ya bongo fleva. Pengo hili la kiutafiti ndilo tatizo ambalo utafiti huu umelishughulikia na kuliziba.

Hivyo basi, utafiti huu umechunguza jinsi kipengele cha tamathali za semi kinavyotumika katika kusawiri suala la ujinsia katika mashairi ya bongo fleva. Jilala (2010) katika makala yake aliyowasilisha katika tamasha la Elimika na Bongo Fleva amejadili juu ya lugha na ujinsia katika mashairi ya bongo fleva kwa kutumia kipengele kimoja tu cha sitiari tena kwa kutumia wasanii wachache, hii inaufanya utafiti wake kuwa mfinyu na hivyo kuhitajia kufanyika kwa utafiti wa kina juu ya usawiri wa masuala ya kijinsia katika mashairi ya bongo fleva. Tamathali za semi zipo nyingi na sitiari ikiwemo. Hivyo basi, tuliona kwamba, kuna haja kubwa ya kufanya utafiti wa kina zaidi katika uwanja huu wa taaluma ya ushairi wa Bongo Fleva. Kwa maana hiyo, utafiti huu ulienda mbali na kwa upana zaidi katika kuchunguza tamathali za semi katika mashairi ya bongo fleva na jinsi zinavyosawiri masuala ya ujinsia katika jamii.

1.3 Malengo ya Utafiti

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza usawiri wa masuala ya kijinsia katika lugha ya mashairi ya bongo fleva nchini Tanzania ili kuonyesha ni jinsi gani lugha inatumika kujadili suala la ujinsia.

1.3.2 Madhumuni Mahsusi

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni mahsusi manne.

1. Kubainisha tamathali za semi katika mashairi ya bongo fleva.
2. Kuonesha jinsi tamathali hizo zinavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme.
3. Kubainisha nafasi ya mwanamke na mwanamme kama inavyosawiriwa na tamathali za usemi za mashairi ya bongo fleva.
4. Kuainisha tofauti baina ya wasanii wa kike na wa kiume katika uteuzi wa tamathali za semi katika kusawiri masuala ya kijinsia.

1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti huu ulikusudia kujibu maswali yafuatayo;

1. Ni tamathali zipi za usemi zinazojitokeza katika mashairi ya bongo fleva?
2. Tamathali hizo zinasawiri vipi mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme?
3. Mwanamke na mwanamme wanapewa nafasi gani katika tamathali za semi zilizotumika katika masahiri ya bongo fleva?

4. Kuna tofauti au kufanana katika kuteua tamathali za semi zinazomsawiri mwanamke baina ya wasanii wa kike na wale wa kiume?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu nne; kwanza, utafiti huu utawasaida wanafunzi wa elimu mitindo, Wanaisimu na wanafasihi kuelewa upekee wa maandishi katika uteuzi wa vipengele vya lugha kiisimu katika ujenzi wa kazi za fasihi hususani katika mashairi.

Pili; utafiti huu utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeleo na pia ni changamoto kwa watafiti kufanya utafiti zaidi katika kazi za fasihi simulizi.

Tatu; utafiti huu ni malighafi, kwani utatoa mchango katika historia ya fasihi simulizi hasa katika ushairi na hatimaye utatajirisha maktaba ya chuo.

Utafiti huu utatoa mchango wa maarifa katika taaluma ya elimu mitindo na masuala ya kijinsia kwa ujumla. Hivyo basi, utatumika kama marejeleo kwa watafiti wengine.

1.5.1 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza tamathali za semi kama kipengele kimojawapo katika lugha. Aidha mashairi ya bongo fleva yapo mengi lakini utafiti huu ulichunguza mashairi ya bongo fleva ya wasanii sita tu yaani wanawake watatu na wanume watatu.

1.6 Vikwazo ya Utafiti

Utafiti huu ulitegemea kukumbana na vikwazo kadhaa; kwanza ni suala la pesa, mazingara na ugeni wa mtafiti katika nchi ya Tanzania. Kimsingi, mtafiti anatokea nchini Libya hivyo mazingira ya Tanzania yalikuwa magumu kwake na pia kuelewa mila na desturi za Watanzania ambayo kwa hakika alijitahidi kutatua vikwazo hivi na kisha kufanikiwa kupata data zilizowezesha kujibu maswali ya utafiti huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Lugha imejengwa na vipengele mbalimbali ambavyo hutumiwa katika kazi za fasihi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Moja ya kipengele cha lugha ni tamathali za usemi. Vipengele mbalimbali vya tamathali za usemi vimejadiliwa na kuwasilishwa katika sehemu hii. Miongoni mwa vipengele vivyo ni tashibisha, sitiari, taswira, ishara, sitiari na taashira. Vipengele hivi vinajadiliwa kwa kina hapa chini kama ifuatavyo:

2.1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Kuu

2.1.2 Tamathali za Semi

Tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza, au kuubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kwamba tamathali zinazotumika zaidi katika ushairi ni tashibiha, tashihisi, kejeli, metonimia na sitiari.

Msokile (1993) anaeleza kwamba, tamathali za usemi ni maneno, nahau au semi ambazo hutumiwa na waandishi wa fasihi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana mtindo na pengine sauti katika maandishi hayo.

Tamathali za usemi zinatumiwa pia kupamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha. Hivyo katika utafiti huu tumechunguza vipengele vya lugha

ambavyo vimejikita katika uhamishaji wa maana kutoka katika dhana moja kwenda nyingine ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

2.1.3 Tashibiha

Tashibiha ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno kama; mithili ya, kama kwamba, kwa mfano; mweusi kama mkaa, mweupe mithili ya theluji, mrefu kama twiga. Mifano hii ni tashibiha kwa sababu inalinganisha vitu vyenye umbo na sifa tofauti kwa kutumia maneno tuliyoyataja katika sehemu hii.

Wamitila (2008) anasema kuwa, tamathali hii ya usemi hupatikana pale ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Tashibiha hutambulishwa na matumizi ya viungo kama; mfano wa, mithili ya, kama vile, na kadhalika, hii ni tamathali inayotumiwa sana katika kazi za kifasihi.

2.1.4 Tashihisi

Tashihisi ni usemi ambao sifa ya uhai huwa imehamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai au dhana dhahania (pengine tashihisi huitwa uhaishaji). Tashihisi hutumiwa zaidi na washairi ambao kwa mfano hawasiti kusema, kimya hakishi kunena, kitakapo kusimamia, fedha huita wazuri wakaitika labeka, maji baridi yaliubusu mwili wake mwororo. Katika mifano hii kimya kimepewa sifa ya kibinadamu ya kunena na kusimamia, fedha imepewa sifa ya kuita na maji yamepewa sifa ya kubusu. Hivyo basi, neno kimya, fedha na maji vimetumika kama tashihisi kwa kupewa uhai. Kinachoonekana hapa ni kwamba sifa za vitu vyenye uhai zimehamishiwa kwenye maneno hayo.

2.1.5 Taashira

Taashira ni tokeo la uhamishaji wa maana ambapo kwa mfano unakuta fungu la maneno linawakilisha kitu, mtu au dhana nyingine yenye uhusiano nalo (Senkoro, 1982). Kwa Mfano, neno ikulu kwa kuwa linahusiana na uraisi hutumika kuwasilisha dhana ya urais, jembe hutumika kuwakilisha ukulima. Vile vile, neno kanga kwa mfano, linaweza kuwakilisha mwanamke.

2.1.6 Ishara

Senkoro (1982:36) anaeleza kuwa, ishara ni dhana au mawazo mbalimbali yanayotumiwa na washairi na wanafasihi mbalimbali katika kazi zao kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine. Katika utafiti huu tumeongelea juu ya ishara[1] zinazopatikana katika mashairi teule ya bongo flava na kuonesha; kwa maoni yetu chini ya nadharia ya Simiotoki zinawakilisha au zinaeleza nini katika muktadha wa kijamii huku tukihusisha na masuala ya kijinsia (Leech, 1960). Kimsingi, tunaamini kwamba uhakiki tulioufanya utawasaidia wasomaji wachanga kupata mwanga wa kuelewa masuala ya kijinsia katika mashairi ya bongo fleva na wanataaluma wabobezi kutambua umuhimu wa vipengele vya tamathali za semi katika kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa.

2.1.7 Taswira

Taswira ni picha wanayoipata wasomaji wa kazi ya fasihi wasomapo kazi husika. Taswira hupatikana kutokana na ishara, sitiari, tashibiha na pengine uhalisia-

---

[1] “Ishara ni neno au usemi wenye maana inayowakilisha dhana nyingine kwa kuhusiana nayo. Yaani, neno au usemi huo huwa na viwango viwili vya maana; maana ya moja kwa moja na maana ya Kitamathali (Kahigi, 1995: 29).”

mazingaombwe (Senkoro, 1982; 2006). Kwa mfano: usomapo riwaya ya *Nagona* (1990) unakutana na mambo mengi ya ajabu ajabu kama vile maiti anaongea na mtoto anaongea akiwa tumboni kwa mama yake. Uajabuajabu huu hutoa picha au taswira ya jambo au mambo fulani katika jamii tuishio. Maana hizo ambazo huweza kuibuliwa kulingana na mwitiko wa msomaji ndiyo picha au taswira tulizozungumzia katika utafiti huu.

2.1.8 Sitiari

Hii ni tamathali ya usemi ambayo kwa kawaida inalinganisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti. Ulinganisho huo unazingatia misingi au sifa inayopatikana au zinazopatikana katika vitu vyote viwili lakini sifa hizo haziwi wazi kati ya kitu na kitu (Lakoff na Johnson 1980). Kwa mfano,

(a) Maisha ni moshi

(b) Mtu kinyonga

(c) Ana mwendo wa kobe

Mfano (a) umefananishwa na moshi. “Moshi” ni kitu kinachodumu kwa muda mfupi sana toka pale unapojitokeza. Kwa hiyo “Mtu” ambaye amefichwa katika neno “Maisha” anaishi kwa muda mfupi sana kama vile maisha ya moshi yalivyo. Mfano (b) unamlinganisha “mtu” na “kinyonga”, kinyonga ni mnyama aliye na tabia ya kubadilika rangi kila awapo katika mazingira mapya. Kutokana na dhana hii mtu anafikiriwa kuwa kinyonga kwa sababu hatabiriki wakati wowote anaweza kubadilika na kwenye mazingira yoyote yale. Ni vema tukaeleza kwamba, sitiari ni

tamathali ya usemi ilinganishayo vitu bila kutumia viunganishi kama vile, mithili ya, mfano wa, sawa na, na kadhalika (Omary, 2010; 2011).

Muundo wa sitiari una vipengele vitatu: kizungumzwa, kifananisho na kiungo (Kahigi 1995). Kizungumzwa ni kitajwa, ambapo katika mfano wetu ni *Hamisa*; kifananishi ni kitu kinachohusishwa na kizungumzwa na katika mfano wetu ni *ua*, na kiungo ni tabia au sifa zinazounganisha kizungumzwa na kifananishi hapa ni uzuri. Huu ndiyo uelewa juu ya sitiari uliotumiwa na mtafiti wa utafiti huu.

2.2 Umuhimu wa Istilahi Tajwa Katika Kazi za Fasihi na Utafiti Wetu

Kwa mujibu wa utafiti huu tunona kwamba, vipengele hivi vina umuhimu mkubwa katika kazi ya fasihi. Kwanza, humfanya msomaji kuwa mzalishaji wa maana katika kazi ya fasihi kuliko kuwa mteja tu. Hii inamfanya msomaji kufikiri juu ya ishara au sitiari fulani huku akijaribu kuhusianisha na mambo mbalimbali katika jamii yake na baadaye kuelewa mwandishi, mtunzi au mwimbaji alikusudia nini[2].

Pili vipengele hivi vya kifasihi simulizi huwapa waandishi uhuru wa kueleza mambo kinagaubaga, pengine kwa sababu wadhibiti hawawezi kuwabana kuwa, kwa nini hapa umeandika hivi au vile? Imetokea kufungiwa kwa baadhi ya kazi za fasihi kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni kwamba, kazi hizo zinakiuka maadili ya jamii. Mfano mzuri wa kazi hizo ni *Rosa Mistika* (1971) iliyofungiwa kutumika katika elimu ya sekondari. Hata hivyo, kutokana na uhuru

[2] Msomaji wa kazi ya fasihi anatumia uzoefu wake, historia yake, utamaduni wake, imani yake kuikabili kazi ya fasihi. Hii ni misingi ya nadharia ya mwitiko wa msomaji.

anaoupata mwandishi kupitia vipengele tajwa hapo juu, Kezilahabi ameweza kuandika mambo yale yale na pengine zaidi ya hayo katika *Nagona* (1990), *Mzingile* (1991), *Kaputula la Marx (1999)*, *Kichomi* (1974), *Dhifa* (2008) na kadhalika (Omary, 2011). Huu ndiyo uhuru apewao mwandishi na vipengele vya ishara, sitiari, taswira na uhalisiamazingaombwe katika kueleza, kuibua na kufichua mambo mbalimbali katika jamii. Tumevichunguza vipengele hivi kwa kina kwa kuwa ni sehemu ya vipengele vya tamathali za usemi vilivyoshughulikiwa katika mashairi teule ya bongo fleva.

2.3 Tafiti Tangulizi Katika Ushairi wa Bongo Fleva

Watafiti mbalimbali wamefanya utafiti kuhusu mashairi ya bongo fleva kwa madhumuni mbalimbali. Wengi wao wamejadili suala la maudhui na baadhi yao kujadili suala la lugha katika mashairi hayo. Majembe (1998) ameandika kuhusu suala la matumizi ya lugha katika muziki wa Hip hop. Katika makala yake hii ameshughulikia suala la kipengele cha kiisimu jamii cha uchanganyaji wa lugha. Anasema kuwa, sifa moja ya mashairi ya bongo fleva ni matumizi ya uchanganyaji wa lugha. Tunaungana mkono na matokeo ya utafiti wake kwamba, wanamuziki wa bongo fleva wanachanganya lugha zaidi ya moja katika nyimbo zao. Ni katika kuchanganya lugha ndipo tamathali mbalimbali za usemi huibuliwa ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira kama ilivyokusudiwa. Mawazo haya yanasukuma mbele utafiti wetu ingawa Majembe (1998) hajashughulikia suala la ujinsia katika bongo fleva. Hivyo basi, utafiti huu umeziba pengo hilo huku ukitumia mawazo yao.

Katika makala yake, Senkoro (2003) anakubaliana na matumizi ya uchanganyaji wa lugha katika bongo fleva. Hata hivyo, ameenda mbali na kuzungumza kuwa wasanii

hutumia mashairi hayo kuelezea matumaini yao, matatizo yao, hisia zao, na matarajio yao. Maelezo ya Senkoro (ameshatajwa) ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu. Tunasema hivi kwa sababu, watunzi na waghanaji wa mashairi ya bongo fleva hutumia tamathali mbalimbali za usemi katika kufikisha ujumbe unaoelezwa na Senkoro (ameshatajwa). Utafiti huu umechunguza kwa kina ni aina gani za tamathali za usemi zinazotumiwa na wasanii wa bongo fleva katika kuwasilisha matamanio, hisia, matarajio na matatizo yao na yale ya jamii. Kwa kufanya hivyo tulionesha ni namna gani masuala ya kijinsia yakifafanuliwa na kuwasilishwa kupitia tamathali hizo yanaweza kuelimisha jamii kwa kiasi kikubwa.

Perullo (2005) katika kazi yake ya “Hooligans and heroes: Youth Identity and Hip-Hop in Dar es Salaam”, akinukuliwa na Omari (2009) anasema kuwa, vijana wanatumia mashairi ya bongo fleva kupamabana na changamoto za kijamii. Wanatumia mashairi hayo kuelimisha watu kuhusu suala la UKIMWI, rushwa, ukosefu wa ajira, matabaka na mambo mengine mengi ya kijamii.

Mawazo haya pia yanamchango mkubwa katika kusukuma mbele utafiti huu kwa kuwa yanadai kwamba, wasanii wa bongo fleva hutumia nyimbo zao kuelimisha na kuasa jamii juu ya mambo mbalimbali. Katika kufanya hivyo, hutumia vipengele mbalimbali vya tamathali za usemi na katika tamathali hizo ndimo masuala ya kijinsia huelezwa na kuwasilishwa kwa jamii husika. Utafiti wetu ulichambua kwa kina mashairi teule ya bongo fleva ili kuonesha namna tamathali za usemi zinavyotumiwa kuwasilishia masuala mbalimbali ya kijinsia katika jamii.

Omari (2006) kama anavyonukuliwa na Omari (2009) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha na mtindo katika hip hop. Katika makala hii anabainisha matumizi ya tamathali za semi kama vile sitiari, tashibiha, taswira, urudiajirudiaji na kadhalika. Pia anaelezea matumizi ya nduni zingine za lugha kama vile matumizi ya anaomatopeia, nyimbo za watoto, uchanganyaji wa lugha na ukopaji wa maneno. Maelezo ya mtafiti huyu yanaonesha kwamba, watunzi na wasanii wa mashairi ya bongo fleva wanatumia sana tamathali za usemi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Hata vivyo, maelezo yake ni madokezo tu ambayo hayaelezi kwa kina juu ya masuala ya kijinsia yanayowasilishwa kupitia tamathali husika. Utafiti wetu umeeleza kwa kina namna tamathali za usemi katika mashairi teule ya bongo fleva yanavyowasilisha masuala ya kijinsia kwa jamii husika.

Naye Jilala (2008) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya kisanii ya sitiari katika ujenzi wa maana na ujumbe katika nyimbo za kizazi kipya. Katika utafiti wake anasema kuwa, sitiari hutumiwa kisanii kujenga maana na ujumbe wa nyimbo za kizazi kipya. Katika utafiti wake huo amejadili pia suala la nafasi ya mwanamke na jinsi inavyojitokeza katika sitiari. Anaendelea kusema kwamba, mwanamke huchorwa kama mama, kiumbe duni na chombo cha kumstarehesha mwanaume. Tunaungana mkono na mawazo ya mtafiti huyu kuhusu namna mwanamke anavyochorwa kupitia sitiari ambayo ni aina mojawapo ya tamathali ya usemi na tunasema kwamba, mawazo haya yamesukuma mbele utafiti wetu. Hata hivyo, katika makala ya Jilala (ameshatajwa) suala la jinsia halijazungumzwa kwa kina kama ilivyoshughulikiwa katika utafiti huu. Hivyo basi, tofauti na utafiti huu wa Jilala utafiti wetu umechunguza kwa kina masuala ya kijinsia na jinsi yanavyosawiriwa katika mashairi

ya bongo fleva kupitia vipengele kama vile ishara, sitiari, taashira, tashibiha na tafsida ili kuweza kuonesha masuala hayo kwa upana zaidi na kupata taswira kamili ya utokeaji wa masuala hayo katika jamii kupitia mashairi ya bongo fleva.

Omari (2009) alifanya utafiti wa shahada ya uzamivu katika bongo fleva kama fasihi pendwa nchini Tanzania. Katika utafiti huu alionesha kwamba, mwanamke bado anaonekana kama chombo cha starehe na ndiyo maana hata mavazi anayovaa mwanamke katika utendaji wa nyimbo za bongo fleva ni ya kiudhalilishaji yanayoonesha sehemu za maungo yake ya ndani. Hii ni tofauti na wanamme ambao huvaa mavazi yenye kusitiri maungo yao.

Mawazo haya yamesukuma mbele utafiti wetu kwa misingi kwamba, masuala ya kijinsia tuliyoyachunguza katika utafiti huu yanaonekana kujitokeza katika ushairi wa bongo fleva (Mangesho, 2003). Hata hivyo, suala la jinsia katika kazi ya Omari (ameshatajwa) limeelezwa kwa ufinyu sana kiasi cha kutoonesha picha kamili ya namna masuala ya kijinsia yanavyojadiliwa na kuwasilishwa katika mashairi ya bongo fleva. Tofauti na kazi ya Omari (2009) utafiti huu umechambua kwa kina masuala ya kijinsia katika mashairi teule ya bongo fleva kupitia vipengele kadhaa vya tamathali za usemi vilivyoteuliwa.

Kwa ujumla ukiangalia watafiti wote hao unaweza kuona kwamba, wamefanya utafiti katika mashairi ya bongo fleva kwa mitazamo tofauti. Hata hivyo, hakuna hata mmoja ambaye amefanya utafiti kuhusu usawiri wa masuala kijinsia katika mashairi hayo.

2.4 Hitimishi

Mapitio ya kazi tangulizi ni kipengele muhimu sana katika kubainisha pengo la kiutafiti ambalo mtafiti anakusudia kulijaza. Katika sura hii tumepitia machapisho mbalimbali ambayo yametuwezesha kufafanua istilahi mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu na kutazama watafiti watangulizi wanaeleza nini kuhusiana na masuala ya kijinsia katika nyimbo za bongofleva. Sura hii imebaini kwamba hakuna utafiti uliofanyika kwa kina katika kuchunguza masuala ya kijinsia yanavyosawiriwa katika nyimbo za bongo fleva. Utafiti huu umefanywa ili kuziba pengo hili la kiutafiti.

SURA YA TATU

NADHARIA YA UTAFITI NA UTEUZI

3.1 Mwega wa Kinadharia

Sura hii inaeleza nadharia kadhaa ziongozazo utafiti wa kifasihi na kisha kuteua nadharia muafaka iliyosaidia kuwezesha kufanyika kwa uhakiki wa masuala ya kijinsia katika mashairi ya bongo fleva kupitia vipengele anuai vya tamathali za usemi. Tunaanza na nadharia ya Umarx

3.2 Nadharia ya Umarx

Msingi mkubwa wa nadharia hii inatokana na mawazo ya Karl Marx na Friedrich Engels. Mwanafalsafa wa Kijerumani Karl Marx (1818-1863) anahusisha U-Marx na nyanja kama vile uchumi, historia jamii na mapinduzi (Wamitila 2002:182). Kimsingi, mawazo ya Marx yanalenga kuwataka wanafasihi kuzitazama hali za jamii zao zilivyo na kuzitafutia ufumbuzi kwa maana ya kuzibadilisha kuliko kuzitafsiri tu.

Mawazo ya Karl Marx kuihusu historia na miundo ya kijamii yana nafasi kubwa katika nadharia hii. Umarx ni falsafa ya kiyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali za kiyakinifu za maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. Marx hautegemezi mfumo wake wa kifalsafa kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto bali anayetegemeza kwenye uhalisi unaoonekana (Wamitila, 2002:182). Mawazo haya yametusaidia kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, mashairi ya bongo fleva huihakiki jamii katika uhalisia na si udhahania kama Kezilahabi, Mkufya na Wamitila, kuwataja wachache. Mfumo wa maisha tulionao leo ni ule ulioongeza

tofauti kati ya walionacho na wasionacho (utabaka) na kusababisha kuwapo kwa mgogoro wa kitabaka katika jamii za Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Kupitia migogoro ya kijamii ndipo masuala mbalimbali ya kijinsia yanapojitokeza na kuwasilishwa kwa jamii kwa njia mbalimbali kama vile mashairi ya bongo fleva. Kimsingi, nadharia ya U-marx ndiyo mahala pake katika kufanikisha uchambuzi wa matabaka ambayo ndani yake kuna masuala ya kijinsia tuliyochambua katika utafiti huu.

Kimsingi, mabadiliko ya mfumo msingi uchumi wa jamii ndiyo hasa hubadili mfumo wa maisha na muundo wa utawala. Kwa mfano, kuanzishwa kwa soko huria kulikochangiwa na utandawazi kumebadili mifumo ya maisha ya jamii na kuleta utabaka uliopita mipaka, yaani usioelezeka. Wamitila (2002:183), anasema:

> Wahakiki wa Ki-Marx wanaamini kuwa daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi-jamii. Itakumbukwa kuwa Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka… Kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mavazi na mambo mengine.

Ni kutokana na mahitaji haya ya msingi ndipo binadamu hupambana na kupigana ili kuhakikisha anayapata ili kuishi maisha mazuri. Hata hivyo, wapo wanaozidisha kipimo na kutamani zaidi kuwazidi wengine na hivyo kuweka tabaka la wenye nacho na wale wasionacho. Hali hii huwafanya baadhi ya wanajamii kufanya ama kushiriki katika matendo yasiyokubalika katika jamii ilimradi wapate fedha za kukimu maisha yao. Kwa kufanya hivyo, kunajitokeza masuala mbalimbali yanayohusiana na masuala ya kijinsia ambayo huwasilishwa katika jamii kupitia mashairi ya bongo

fleva. Utafiti huu umeyachambua masuala haya kwa kina kama inavyoonekana katika sura ya nne ya utafiti huu.

Vile vile, wenye nacho huendelea kupambana ili kuhakikisha wanaendeleza utajiri wao daima na kamwe wasishuke chini. Katika kutimiza lengo lao hili dhalimu hujikuta wakiwanyonya, wakiwadhulumu na kuwakandamiza wasio nacho. Unyonyaji huu unaweza kujidhihirisha katika masuala ya rushwa, kuwanyang'anya wananchi ardhi kwa maslahi ya wachache na pato la taifa kufaidisha wachache badala ya wengi, yaani jamii nzima. Mambo haya hayafanywi na mtu wa chini katika jamii. Ukweli huu si tu kwamba, unaongeza umasikini nchini bali unakuza utabaka katika jamii.

Masuala ya kijinsia yanayoonesha utabaka juu ya mambo mbalimbali kati ya wanaume na wanawake hususani kielimu, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni yanayoelezwa katika mashairi ya bongo fleva yanaweza kuchambuliwa vizuri kupitia nadharia ya Umarx. Hivyo basi, nadharia hii ilituongoza vema katika uchungunzi na uchambuzi kuhusu masuala ya kijinsia katika mashairi teule ya bongo flava.

3.2 Nadharia ya Simiotoki

Simiotiki ni nadharia inayoshughulika na ishara, picha, sitiari, taswira pamoja na misimbo mbalimbali katika kazi za fasihi. Waandishi hutumia ishara za aina mbalimbali katika kueleza jambo kwa jamii kupitia sanaa, fasihi ama filamu (Wamitila 2002). Kuibuka kwa nadharia hii kunahusishwa sana na nadharia ya umuundo iliyoasisiwa na Ferdnand Dessaussure na kuwekewa misingi yake katika fasihi na Barthes (1994) anayedai kuwa huwezi kuchambua matini kivyake vyake,

kwani hakuna matini inayojitegemea yenyewe, bali kuwepo kwa matini moja kunaashiria kuwepo kwa matini iliyoandikwa kabla. Kwa mfano, uandishi wa aina ya *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) umeathiriwa sana na kazi kama *Kusadika* (1951*), Kufikirika* (1967), *Mashetani* (1971), *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* (1976) ambazo nazo hazikutumia mandhari halisi. Hivyo, *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) ni mwendelezo wa hali ya juu kabisa wa kazi hizo zilizotangulia. Mashairi ya bongo fleva nayo yameathiriwa na kuathiriana na kazi mbalimbali za kifasihi na hata zisizo za kifasihi. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki tumeweza kudadavua tamathali mbalimbali za usemi na kueleza kwamba zinaeleza nini kuhusu masuala ya kijinsia ambalo ndilo lengo kuu la utafiti huu.

Hivyo basi, katika kufanikisha lengo la utafiti huu, nadharia ya Simiotiki ilikuwa muhimili muhimu katika kuainisha ishara, picha, taswira, tashibiha na sitiari katika mashairi teule ya bongo fleva ili kuibua masuala mbalimbali ya kijinsia yanayowasilishwa kupitia mashairi hayo.

3.3 Nadharia ya Ufeminist

Nadharia nyingine ni ile ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike (Feminist Psychoanalytic Theory). Hii ni nadharia iliyoibuka kutokana na kazi zilizoasisiwa na Jacques Lacan kama alivyonukuliwa na Momanyi (2001). Nadharia hii kimsingi inasaidia kuhakiki matini katika misingi ya uchanganuzi nafsia ambao hutazama zaidi tabia na mwenendo na mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Vile vile, nadharia hii huzingatia kuweko kwa nafsi bandia au nafsi isiyo halisi iliyojengwa

kutokana na mielekeo ya kiuana, utaratibu fiche wa kisaikolojia pamoja na taasubi za kiume.

Katika utaratibu fiche, maumbo halisi ya kiisimu katika akili ya mwanamke hughubikwa na badala yake maumbo ya kidhahania huimarishwa. Maumbo haya yasiyo na uhusianao wowote na uhalisia wake kama binadamu ndiyo yanayobainika hususani kupitia lugha na tabia yake. Utaratibu huu ambao ni wa kiishara ndio unaoashiria tofauti za kiuana zinazopatikana katika utamaduni wa jamii.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, nafasi ya mwanamke imefungamana na lugha inayomzungumzia, lugha inayoashiria uana wake. Nafasi hii hufinyangwa na jamii kupitia asasi mbalimbali ili aweze kukubalika katika utaratibu huo wa kiishara. Uchanganuzi nafsia katika mtazamo wa kike basi, ni nadharia bia ya uumbaji wa nafsi katika misingi ya uana.

Sababu ya kuteua nadharia hii, ni kwamba wapo watafiti ambao pia wametumia nadharia hii katika kuchambua mahusiano ya mwanamke na mwanamume katika kazi za fasihi wakiongozwa na Momanyi (2001; 2007). Hivyo basi, nadharia hii imekuwa mhimili mkubwa katika kuchambua na kuchunguza masuala ya kijinsia katika mashairi ya bongo fleva kama ilivyowasilishwa katika sura ya tano ya tasinifu hii.

Katika muktadha wa uchambuzi wa matini za mashairi ya bongo fleva, nadharia hii inaweza kutumiwa kwa kuzingatia kwamba, lugha haiwakilishi uhalisia bali ni utaratibu wa kiishara. Hivyo taswira za wanawake katika fasihi aghalabu

haziwakilishi uhalisi wao bali ni taswira bandia zilizosheheni ishara za uana, hususani katika matumizi ya lugha. Aidha uhakiki huo una wajibu wa kuzingatia kuwepo kwa taasubi za kiume zilizoimarishwa ndani ya utaratibu wa kiishara katika mfumo wa kuumeni. Taasubi hizo ndizo zinazomdunisha mwanamke na kumweka katika kitengo maalumu kijamii na kumuimarisha mwanamke (Momanyi, 2001). Nadharia hii imetumika pia kujadili jinsi lugha ya kiishara inavyotumika kuonesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanamume katika jamii.

Kwa kutumia nadharia hii pia tumeonesha jinsi gani mwanamke anachorwa kiishara kwa kutumia lugha. Aidha tumejadili ishara ambazo zinaibuka kutokana na lugha iliyotumika katika mashairi ya bongo fleva.

3.4 Hitimishi

Nadharia ya utafiti ni kiongozi muhimu katika kuufanya utafiti uweze kukamilisha malengo yake kama inavyopasa. Katika utafiti huu nadhari za Umarx, Simiotiki na Ufeministi wa Kisaikolojia ndio zilizotumika katika kusaidia uchambuzi wa data kama unavyoonekana katika sura ya tano ya tasinifu hii. Nadharia hizi kwa pamoja zimeweza kuonesha kuibua masuala mbalimbali ya kijinsia kama yanavyojitokeza katika nyimbo za bongo fleva zilizoteuliwa.

SURA YA NNE

MBINU ZA UTAFITI

4.1 Njia za Kufanyia utafiti

Sura hii inaeleza juu ya mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Mbinu hizo ni kama zifuatavyo:

4.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani ambapo kazi za wasanii sita wa muziki wa bongo fleva ziliteuliwa na kuchunguzwa ili kubainisha namna zinavyozungumzia masuala ya kijinsia kupitia tamathali mbalimbali za usemi. Vile vile, utafiti huu ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam ambapo ndipo wasanii teule wanapopatikana. Kothari (2008) ameubainisha uchunguzi kifani kama ni mpango au mpangilio unaonesha jinsi na namna data zilivyokusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia gharama nafuu. Isaack na Michael (1981) na Creswell (2009) wanasema kwamba, uchunguzi kifani hutoa fursa ya kuchunguza jambo kwa undani zaidi na kuhusisha vipengele mbalimbali vinavyounda ama kujenga jambo hilo. Robson (2007) na Yin (1994) wanahitimisha kwamba, mbinu ya uchunguzi kifani husaidiya kupatikana kwa majibu ya maswali kama vile: Nini? kwa nini? Kwa vipi? Na kwa sababu gani? Na kadhalika. Kothari (2008) anakazia kwa kusema kuwa, uchunguzi kifani humuwezesha mtafiti kuelewa muktadha na mahudhuriyo mazima ya utokeaji na utendekaji wa jambo fulani katika jamii. Hivyo basi, uchunguzi kifani ulitusaidia kuchunguza kwa kina masuala ya kijinsia katika mashairi ya bongo fleva ya wasanii teule.

4.3 Eneo la Utafiti

Kothari (2008) anaeleza kwamba, eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti husika unapofanyikia ukihusisha watafitiwa ama vitafitiwa. Hivyo basi, eneo la utafiti ni jiji la Dare es salaam. Mtafiti alitembelea katika matamasha yaliyokuwa yameandaliwa na wasanii husika ili kufanya nao mahojiano pamoja na kushuhudia namna tamathali za usemi zielezazo masuala ya kijinsia zinavyowasilishwa jukwaani katika kumbi mbalimbali zilizopo jijini Dar es Salaam. Sababu kubwa ya kuteua eneo hili kwanza ni jiji ambalo viwanda na makampuni ya kurekodia mashairi ya bongo fleva yanapatikana. Pili, wasanii wengi kutoka mikoani wamehamia na kufanyaia kazi zao katika jiji hili kitu ambacho kilituwezesha kupata uwakilishi mzuri wa Watanzania na hivyo kupata picha kamili ya mitazamo na misimamo mbalimbali juu ya masuala ya kijinsia katika jamii. Tatu, Dar es Salaam ndiyo soko kuu la kazi za wasanii wa bongo fleva na hivyo ni rahisi kupata kazi za wasanii teule katika utafiti huu.

4.3.1 Kundi lengwa

Kulingana na Yin (1994) anaeleza kwamba kundi lengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Uteuzi wa kundi lengwa hufanywa huku mtafiti akitambua kwamba, kundi hilo litampatia data zitakazokidhi malengo ya utafiti wake. Kwa hiyo katika utafiti huu walengwa ni wasanii wa bongo fleva na hadhira yake.

4.4 Usampulishaji na Sampuli

4.4.1 Usampulishaji

Mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa hujulikuana kama mbinu ya usampulishaji. Kwa vile siyo rahisi kukusanya taarifa zote kutoka kwenye kundi

zima, basi mbinu ya usampulishaji yenye madhumuni maalumu na mbinu ya sampuli nasibu zilitumika kuteua watafitiwa katika utafiti huu. Sampuli nasibu ni ile inayotoa nafasi sawa kwa kila memba kuteuliwa kama sampuli katika utafiti husika. Mbinu hii ilitumika kuteua wasikilizaji na wapenzi wa kazi za wasanii teule katika utafiti huu. Mbinu yenye madhumuni maalumu ni mbinu ya usampulishaji ambayo humpa mtafiti uhuru wa kuteua watafitiwa ama vitafitiwa ambavyo anaamini kwamba vitampatia data muafaka kulingana na malengo ya utafiti husika (Kothari, 2008). Mbinu hii imetumika kuteua wasanii na kazi zao ambazo zimeshughulikiwa katika utafiti huu. Wasanii hao walikuwa sita wakijumuisha wanaume na wanawake.

4.4.2 Sampuli

Sampuli ni istilahi inayotumika kumaanisha vitu au watu walioteuliwa kujibu maswali ya utafiti kutoka katika kundi kubwa la vitu au watu waliopo katika eneo la utafiti (Kothari, 1990). Katika utafiti huu siyo rahisi kuhusiha wasanii wote wa bongo fleva na wasikilizaji na wapenzi wote wa bongo fleva. Hivyo basi, katika makundi hayo, mtafiti aliteua sampuli wakilishi ambayo iliwezesha kupatikana kwa data zilizoweza kujibu maswali ya utafiti huu.

4.4.2.1 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli kama unavyoelezwa na Robson (2007) ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilisho cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Zipo mbinu mbalimbali za uteuzi wa sampuli lakini sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia njia mbili, yaani *uteuzi bahatishi* na *uteuzi wa madhumuni maalumu*. Hivyo basi, mtafiti aliteua jumla

ya watafitiwa 66 na kuwapatia hojaji ambazo walizijaza na kuzirudisha kwa mtafiti. Hivyo basi sampuli iliteuliwa kulingana na sifa za kijinsia, umri, kazi na kiwango cha elimu. Sababu ya kuamua kutumia vigezo tajwa katika kuteua sampuli ni ili kuwezesha kupata data muafaka zilizosaidia kukamilisha malengo ya utafiti wetu.

4.4.2.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Uteuzi wa madhumuni maalumu ni mbinu ya uteuzi wa watafitiwa ambapo mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake (Kothari, 2004). Kimsingi, Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba, mtafiti ana taarifa juu ya uwepo wa hadhira na wasanii wa bongo fleva. Hivyo basi, mtafiti anaamini kuwa kundi hilo ndilo walengwa wanaoweza kutoa data za mashairi ya bongo fleva na kwa sababu wao ndiyo hutunga na kuimba mashairi hayo. Vile vile, mtafiti anaamini kuwa utafiti huu unawategemea watu hao ili kupata data toshelevu.

4.4.2.3 Uteuzi Nasibu

Babbie (1999) anaielezea mbinu hii kuwa ni mbinu ambayo hutumia watu ambao ni hadhira tekwa, yaani watu ambao mtafiti anakutana nao bila kutarajia. Katika mbinu hii wahojiwa huwa ni wale watu ambao hutokea wakiwa wanapita au wanaonesha kupendezwa na utafiti husika. Sababu ya msingi ya kutumia mbinu hii ni kwamba, upo uwezekano kwamba isiwe rahisi kupata wahojiwa ambao watakuwa tayari kutoa data hasa katika maeneo ambayo hakuna mwamko wa kielimu na hivyo sampuli nasibu ndiyo muafaka. Hivyo basi, mtafiti alitumia mbinu hii kuwashirikisha hadhira ambayo alikutana nayo uwandani kwa wakati na muktadha wa utafiti.

Hivyo basi, kutokana na sampuli hiyo, kutakuwa na wahojiwa wa kudumu takribani 66. Sababu ya kuteua kuwa na idadi hii ya wahojiwa ni kutaka kupata data toshelevu na hatimaye kufanya majumuisho ya matokeo ya utafiti kutokana na sampuli hiyo. Mchangunuo wa wahojiwa ni kama ifuatavyo;

Kielelezo namba 1: Mchanganuo wa Wahojiwa

WAHOJIWA	**JINSI**		**JUMLA**
	Ke	**Me**	
Wasanii	01	05	06
Hadhira	30	30	60
JUMLA KUU			**66**

Chanzo: Mtafiti, 2012

4.5 Ukusanyaji wa Data

4.5.1 Mbinu za Utafiti

Katika kukusanya data za utafiti huu, mbinu tatu za ukusanyaji data zilihusishwa ambazo ni; mbinu ya usaili, mbinu ya majadiliano na maktaba. Mbinu hizi zilitumika katika kukusanyia data za msingi na data za upili. Tuanze na mbinu ya usaili.

4.5.1.1 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa watafitiwa ana kwa ana na mtafiti au msaidizi wake. Kulingana na Kothari (1993) mbinu hii inaruhusu unyumbukaji katika mchakato wa kuuliza maswali, inamruhusu mtafiti kuuliza maswali ya ziada na wakati huo huo husaidia kugundua mahusiano magumu yaliyopo katika mahusiano ya kijamii. Hivyo basi katika utafiti huu mbinu ya usaili ilitumika ili kupata data za msingi zinazohusiana na malengo mahususi ya utafiti huu. Hata hivyo, kwa mujibu wa Babbie (1999) anaeleza kwamba, kuna aina mbili

za usaili ambazo ni usaili funge na usaili maalumu uliowazi. Utafiti huu ulitumia mbinu ya usaili maalumu uliowazi ambao hutoa fursa ya kufanyika mahojiano ya kina baina ya mtafiti na mtafitiwa.

4.5.1.2 Usaili Maalumu Uliowazi

Mtafiti alitumia mbinu ya usaili maalumu uliowazi ambapo wasailiwa waliulizwa maswali ya msingi ya aina moja na yaliyo katika mpangilio ulio sawa. Mbinu hii ya utafiti ilitoa fursa kwa mtafiti kuuliza maswali yenye kuhitajia maelezo ya kina kutoka kwa watafitiwa juu ya masuala ya kijinsia yawasilishwayo na tamathali za usemi katika mashairi ya bongo fleva. Mbinu hii humuweka mtafiti karibu na watafitiwa na hivyo kuusoma muonekano wao wakati wanapojibu maswali mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti ambapo bila shaka ilinisaidia katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Young (1984) anasema kwamba, mbinu ya usaili maalumu uliowazi ni mbinu ya uhakika katika kusaidia upatikanaji wa data kwa haraka zaidi kuliko mbinu nyingine yoyote ile. Hivyo basi mbinu hii iliniwezesha kukusanya data za msingi kutoka kwa wasanii wa nyimbo za bongo fleva walioteuliwa.

4.5.1.3 Mbinu ya Majadiliano ya Kundi Lengwa

Majadiliano ya kikundi lengwa ni mbinu ambayo hutoa fursa kwa mtafiti kuendesha mjadala na watafitiwa juu ya maswali mbalimbali yahusianayo na mada ya utafiti ili kupata data za msingi (Young, 1984). Majadiliano ya kikundi lengwa yaliandaliwa na kuhusisha kundi la hadhira na wapenzi wa muziki wa kizazi kipya kwa kujumuisha watafitiwa wenye sifa tofauti tofauti za kielimu, kiumri, jinsia na dini.

Mbinu hii ilisaidia kuelewa mtazamo, hisia, maoni na mielekeo ya wahojiwa kuhusu masuala ya kijinsia katika jamii na upokezi wake wa mashairi ya bongo fleva.

4.5.1.4 Mbinu ya Maktaba

Mbinu ya ukusanyaji data maktabani huhusisha ukusanyaji wa data kupitia katika maandiko na machapisho mbalimbali kama vile vitabu, makala, tasinifu, barua, nyaraka na taarifa mbalimbali zilizopo katika mtandao na wavuti (Kothari, 2008). Kwa kutumia mbinu hii, mtafiti aliweza kubainisha vipengele mbalimbali vya tamathali za usemi ambavyo vimetumika katika mashairi teule ya bongo fleva kwa minaajili ya kuyafanyia uchambuzi. Hivyo basi, mashairi teule ya bongo fleva yalisomwa na kuchunguzwa kwa makini ili kuwezesha kukusanya data ambazo ziliwekwa katika shajara maalumu kulingana na darajia. Tunapozungumza juu ya darajia tunamaana ya kila tamathali ya usemi kati ya zilizochaguliwa ilidondolewa katika mahali pake ili kurahisisha zoezi la uwasilishaji na uchambuzi wa data.

4.6 Zana za Kukusanyia Data

Zana za kukusanyia data ni vifaa ama vyombo ambavyo hutumika kama nyenzo za kukusanyia data. Kothari (2001) anasema kwamba, zana za kukusanyia data ndiyo nyenzo muhimu zinazowezesha kupatikana kwa data za utafiti. Hivyo basi, ukusanyaji wa data katika utafiti huu ulihusisha zana zifuatazo.

(i) Matini

Matini tunazozizungumzia hapa ni matini andishi za mashairi ya bongo fleva ambazo mtafiti alizikusanya ili kupata data alizokusudia.

(ii) Kompyuta na Notibuku

Hapa tunapozungumzia kompyuta tunarejelea kompyuta ya mkononi yenye programu ya kinasa sauti na notibuku za kuandikia kumbukumbu. Zana hizi ni muhimu sana katika kukusanyia na kuhifadhi data za awali kipindi cha mazungumzo. Zana hizi za utafiti kwa pamoja zilitumika kukusanya na kurekodi data zilizohusiana na dhana za mashairi, masimulizi ya maana za kiishara, dhima zake na umuhimu wake.

(iii) Vinasa Sauti

Vinasa sauti vilitumika kurekodi sauti wakati wa mazungumzo baina ya mtafiti, hadhira na wasanii. Hivyo basi kwa kufanya hivi mtafiti aliweza kupata data zilizohusiana na mwelekeo wa jamii kuhusu suala la jinsia katika mashairi ya bongo fleva na sababu za uteuzi wa maneno katika mashairi hayo.

(iv) Video Kamera na Kamera ya Kawaida

Video kamera ilitumika katika kurekodi na kuchukua matukio katika muktadha na mazingira ya utafiti. Vile vile, katika kipindi cha mahojiano baina ya mtafiti na wasanii na hadhira kifaa hiki kilitumika. Pia kamera ya kawaida ilitumika kuchukua picha za aina mbalimbali katika eneo la utafiti kwa minajili ya kurahisisha uchambuzi wa data.

(v) Dodoso

Madodoso mawili ya maandishi yaliandaliwa kwa ajili ya wahojiwa. Dodoso la kwanza liliwalenga wasanii teule wa mashairi ya bongo fleva. Dodoso la pili liliwalenga wasikilizaji na wapenzi wa mashairi ya bongo fleva kwa nia ya

kuchunguza upokezi wao juu ya masuala ya ujinsia na usawiri wake katika mashairi ya bongo fleva kupitia majadiliano ya kikundi lengwa.

4.7 Uchambuzi wa Data

Kama ilivyokisha elezwa hapo awali kwamba utafiti huu ni ule usio wa kiidadi wenye kuhitajia maelezo zaidi kuliko mahesabu na takwimu. Kwa msingi huo basi, zipo mbinu mbalimbali zinazotumika kuchambua data za utafiti wa aina hii. Hata hivyo, data ya utafiti huu ilichambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, yaani *uchambuzi wa kimaudhui* na *uchambuzi linganishi*. Uchambuzi maudhui inaelezewa na Babbie (1999) kuwa ni mbinu ya uchambuzi ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana. Dhana kuu au dhamira kuu hubainishwa na kuwekwa pamoja. Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba itasaidia kuweka maana zote zinazohusiana kutokana na data za dodoso na usaili ili kutoa mawazo ya jumla kulingana na malengo ya utafiti huu. Kwa upande mwingine, uchambuzi linganishi hutumika kulinganisha data kutoka kwa watu tofauti.

Katika kuchambua data mtafiti alifanya yafuatayo;

- Kubainisha tamathali za semi katika mashairi ya bongo fleva.
- Kuchambua jinsi tamathali hizo zinavyosawiri ujinsia na maana zilizobebwa na tamathali hizo.
- Kuchambua na kuwasilisha data zilizopatikana katika hojaji, doodso na usaili kwa kutumia mkabala wa kidhamira.
- Kubainisha na kuelezea kutofautiana au kufanana kwa wasanii wa kike na wale wa kiume katika uteuzi wa tamathali za semi kuashiria ujinsia.

4.8 Uhalali na Kuaminika kwa Mbinu za Utafiti

4.8.1 Uhalali wa Mbinu za Utafiti

Uhalali wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika (Cohen na *Wenzake*, 2000). Ili kufanikisha upatikanaji wa data sahihi mtafiti aliongozwa na mbinu tatu za ukusanyaji wa data na nadharia tatu za uhakiki wa kifasihi. Usahihi wa mbinu na nadaria hizo unatokana na ukweli kwamba, mapungufu ya kila moja hukamilishwa na ubora wa mbinu nyingine. Vile vile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake, wanataaluma waliohudhuria katika mawasilisho ya semina na hata wale waliokosa fursa ya kuhudhuria nao walitoa maoni yao juu ya uhalali wa mbinu za utafiti huu baada ya kusoma pendekezo langu la utafiti.

4.8.2 Kuaminika kwa Data

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa/kuzalisha matokeo yaleyale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Best na Khan, 2006). Kuaminika hujitokeza pale ambapo kuna kuwa na uhusiano/ulingano katika taarifa zilizotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti (Furlong na Lovelace, 2000). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kumehakikiwa kwa kutumia mbinu tatu za kukusanyia data na nadharia tatu za uhakiki wa kifasihi zinazo kusudiwa kutoa jibu moja.

4.9 Maadili ya Utafiti

Miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa kuzingatia mtafiti ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti pamoja na kutunza siri za watafitiwa

(Kumar, 1999). Hivyo basi, katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data. Kwa kuwa utafiti wetu ni wa maskanini na maktabani tulihakikisha kuwa dondoo kutoka mashairi teule yanadondolewa kwa usahihi. Kwa upande wa maskanini tulihakikisha kwamba majadiliano na usaili baina ya mtafiti na watafitiwa inabaki kuwa ni siri kati yao na data zilizokusanywa zimetumika kwa ajili ya utafiti wa kitaaluma tu na si vinginevyo.

4.10 Hitimishi

Sura hii imewasilisha mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti na kuonekana kama zinavyoonekana katika sura ya taano ya tasinifu hii. Miongoni mwa mbinu zilizowasilishwa ni zile za kukusanyia data uwandani kama vile usaili na hojaji na ile ya maktabani. Kwa upande wa sampuli ya utafiti iliyotumika ni sampuli lengwa na nasibu. Uchambuzi wa data umefanywa kwa kuongozwa na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo.

SURA YA TANO

UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA

5.1 Utangulizi

Sura hii imefanya uwasilishaji wa data za utafiti ili kujibu maswali ya utafiti na kukidhi madhumuni mahususi ya utafiti huu. Sura hii imebaini kwamba, masuala ya kijinsia yanasawiriwa kwa uhalisia ule uliopo katika jamii bila upendeleo wowote. Hili linadhihirika pale msanii wa kike anapomchora mwanamke kama anavyotazamwa katika jamii bila kufichaficha mambo. Na wasanii wanaume nao wanamsawiri mwanaume na mwanamke kama hali ilivyo katika jamii. Nadharia ya ufeminist, Umarx na Simiotiki zimesawiriwa vilivyo katika sura hii ambayo kwayo ndiyo madhumuni mahususi ya utafiti wetu tumeweza kuyakamilisha. Ufuatao ni uwasilishaji, uchambuzi, matokeo na mjadala wa data za utafiti.

5.1.1 Masuala ya Kijinsia Katika Mashairi ya Bondo Fleva

Mashairi ya bango fleva yamesheni mawazo mengi yanayoeleza masuala ya kijinsia hasa yanayowahusu vijana na jamii kwa ujumla. Masuala hayo; yapo yanayowahusu vijana wa kike na yale yawahusuyo vijana wa kiume. Kwa ujumla, masuala hayo yanaelezwa katika muktadha wa kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Katika sehemu hii tunayoeleza masuala hayo kwa undani na kuyafanyia uchambuzi wa kina. Tunaanza na uchambuzi wa data unaohusiana na masuala ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme kama ifuatavyo:

5.1.2 Sifa ya Mwanamke Dhidi ya Mwanaume

Mwanamke hupambwa kwa kutumia sifa za aina mbalimbali katika jamii kupitia mashairi ya bongo fleva sifa hizo ni chanya na nyingine ni hasi. Msanii maarufu wa

muziki wa bongo fleva anayejulikana kwa jina la Lad Jaydee kupitia wimbo wake wa wanaume kama mabinti anasema,

Wanakula kunywa na kuvaa,
Siku zinaenda,
Vya bure hupenda kupewa,
Wala hamna fikira,
Wanaume kama mabinti.

Tutazamapo dondoo tajwa hapo juu tunakutana na sifa mbalimbali zinazompambanua mwanamke na mwanaume katika jamii. Msanii anadai kwamba, mwanamke ndiye anayestahili kula na kupewa vitu vya bure na si mwanaume. Hili linathibitishwa na msitari usemao*; wanakula kunywa na kuvaa …. Wanaume kama mabinti*, Mwanamke anapaswa kukaa nyumbani, kusubiri mumewe ama mchumba wake amletee kila kitu. Naye bila shaka apokee vitu hivyo na kuvitumia bila hata ya kujaribu kufikiria tu, vitu hivyo vimepatikana vipi. Kwa mabinti, huyo mwanamume anayekaa tu na kusubiri kuletewa kila kitu anafananishwa na mwanamke kupitia tashibiha "Wanaume *kama mabinti*" katika dondoo hapo juu.

Si hivyo tu bali pia, dondoo linaonesha kwamba, mwanamke si kiumbe mwenye uwezo wa kufikiri. Hawezi kamwe kukaa chini na kupanga mipango yake ya maendeleo na jinsi atakayoweza kujikwamua kupitia mipango yake binafsi badala yake anasubiri kupangiwa kila kitu na mwanamume. Hili linathibitishwa na msitari usemao: *Vya bure hupenda kupewa, wala hamna fikira … Wanaume kama mabinti*.

Kimsingi, msitari huu unaonesha kwamba, mwanaume anapaswa kuwa ni mtu wa kufikiri juu ya kila jambo afanyalo ama afanyiwalo lakini mwanamke hapaswi

kufikiri juu ya kila afanyiwalo ama afanyalo. Mawazo haya yanasukuma mbele zaidi utafiti wetu pale Lad Jaydee anaposema;

> … Kila upande wanafiki,
> Siku zinaenda,
> Vya bure hupenda kupewa,
> Wala hamna fikira,
> Wanaume kama mabinti,

Dondoo hili linadai kwamba, wanawake ndio wenye sifa ya unafiki na si wanaume. Unafiki ni sifa mbaya sana kwa jamii na sifa hii anaweza kuwa nayo mwanaume na mwanamke vilevile. Hata hivyo, kwa kuwa ni sifa mbaya basi mwanamke ndiye hupewa na kunaisibishwa nayo zaidi kuliko wanaume. Tunayosema haya kwa sababu, mtunzi na mwimbaji wa wimbo huu ni mwanamke ambaye asingetegemewa kutunga na kuimba wimbo wa aina hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa jamii inamtazama mwanamke kwa mtazamo huo, basi hata wanawake hao ambao ni sehemu ya jamii huathiriwa na kujikuta wakihubiri sifa mbaya kwao badala ya kuzipinga.

Hali hii kwa hakika ilinisukuma kuwauliza watafitiwa kulikoni msanii wa kike kutunga na kuimba wimbo kama huu ambo unatoa sifa hasi kwa mwanamke? Mtafitiwa mmoja alijibu kwamba:

> Mwanamke ni mwanajamii ambaye anaathiriwa na mfumo mzima wa maisha ya jamii alipozaliwa na kukulia. Kama katika jamii yake mwanamke anadharauliwa na kukashifiwa basi naye atajengeka hivyo hivyo na hataona taabu ya kumshusha thamani mwanamke mwenzake. Vile vile, wakati mwingine anafanya hivyo bila kuutambua anamdhalilisha mwanamke mwenzake pamoja na wenzake.

Mawazo haya yanasukuma mbele utafiti wetu kwa kuwa yanashadidia hoja kwamba, masuala ya kijinsia katika jamii huundwa na kuasisiwa na wanajamii wenyewe (Omary, 2011). Tunakubaliana na mawazo ya wanataaluma hawa kwa asilimia mia

kwa mia kwamba, jamii ndiyo hujenga mahusiano ya wanajamii wake na kinachofanywa na wasanii wa bongo fleva ni kusawiri hali halisi ya maisha katika jamii husika. Baada ya kuona namna msanii Lady Jaydee aliyosawiri masuala ya kijinsi kupitia dondoo lake tulilolidondoa hapo awali, sasa tutazame mwedolezo uleule wa kumsawiri mwanamke na mwanaume kutoka kwa wasanii wajulikanao kama Uswahilini Matola na wimbo wao wa *Kosa la Marehemu Baba.*

Wasanii hawa wanasawiri masuala ya Kijinsia kupitia wimbo wao wa UKIMWI pale wanaposema:

> Kosa la marehemu sio kuvaa kondomu
> Bali kosa la marehemu ni kuzini na mademu
> Kabla ya Kifo alikuwa na mademu
> kibao na hao mademu zao
> walikuwa na mabwana kibao na
> hao mabwana zao walikuwa
> na wake zao, nao wakaongeza
> mtandao kwa mabuzi yao
> tena hao nao ni makosa yao.
> Mitego ya bure, mbele
> ya macho ya yoyote, maana
> kazi ya Malaya
> ni kudondosha asali mbele
> ya midomo ya watu, ni laini
> maneno yao kuliko vyote
> lakini mwisho wake ni
> mchungu kuliko shubiri
> na mkali kama upanga
> wenye makali kuwili.

Tutazamapo mawazo yaliyopo katika dondoo hapo juu tunabaini masuala mbalimbali ya kijinsia yanajitokeza. Kwanza, wasanii hawa wanasema, *kosa la marehemu sio kuvaa kondomu bali kosa la marehemu ni kuzini na mademu wengi*. Sentensi hii inaonesha kwamba, wanawake ndiyo hasa wanaojihusisha na masuala ya zinaa kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na wanaume. Huyu marehemu hakuwa na

mwanamke mmoja bali wanawake wengi. Pili, kwa upande mwingine msitari huu unaonesha kwamba, wanaume nao wapo ambao si waaminifu kiasi cha kuweza kuzini na wanawake wengi bila kujali athari zitokanazo na tendo hilo. Kwa kufanya hivi, marehemu alionekana kuwa ni mtu shupavu na mashuhuri lakini baadaye ushupavu na umashuhuri wake ulizimika kama taa baada ya kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kisha kufariki dunia (Mutembei, 2009).

Dondoo hapo juu linaendelea kushadidia kwamba, *marehemu alikuwa na mademu kibao na hao mademu zao walikuwa na mabwana kibao na hao mabwana zao walikuwa na wake zao, nao wakaongeza mtandao kwa mabuzi yao*. Sitiari *Kibao* katika madokezo hapo juu inaashiria wingi uliopita kiasi. Wingi huu unaonekana zaidi kwa mwanamke kuliko mwanaume ingawa wote wanashiriki katika kufanya zinaa. Si hivyo tu, bali pia katika kuendelea kuonesha kwamba, mwanamke ni muhuni na mzinifu na ndiye anamsababishia mwanaume kuingia katika zinaa tunaelezwa kwamba, maana *kazi ya Malaya ni kudondosha asali mbele ya midomo ya watu*. Hapa msanii anatumia neno *asali* kisitiari kurejelea mavazi anayovaa mwanamke kuwa ni yenye kuonesha sehemu za maungo yake ambayo kwayo humtamanisha mwanamme na kujikuta ameingia katika vitendo vya zinaa. Baada ya kuoneshwa asali hiyo baadhi ya wanaume huikimbilia na kuilamba na ndipo tunapoelezwa kwamba, lakini *mwisho wake ni mchungu kuliko shubiri na mkali kama upanga wenye makali kuwili.* Mtunzi anatumia tashibiha “mkali kama upanga…” kuonesha hatari ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa wahusika na madhara yake ambayo ni kuugua na kuteseka kwa muda mrefu, kuongeza umasikini, na kisha kupoteza uhai.

Vile vile, katika dondoo hapo juu inaoneshwa kwamba, wake za watu nao wanatoka nje ya ndoa zao na kusababisha waume zao kupata UKIMWI. Hata hivyo, hao wanaume wanaotembea na wake za watu hawaonekani kukemewa kwa ukali kama wanavyokemewa wanawake. Kwa msingi huu, tunabaini kwamba masuala ya kujamiiana na makosa yake mengi, husukumwa kwa mwanamke na mwanaume kuonekana kutamanishwa tu na si yeye ndiye mkosaji. Nilipenda kupata ufafanuzi zaidi kutoka kwa wahojiwa kuhusu kwanini hali iko hivyo? Mtafitiwa mmoja alidondolewa akisema:

> Wanaume hujikuta wanamtaka mwanamke kimwili na wanawake wengi hawakatai. Kwa hiyo, unakuta mwanamke mmoja katembea na wanaume hata kumi kwa sababu anavaa nguo za kuwatamanisha wanaume na kila anayetamani akimuomba anakubaliwa. Hatua ya hali hii ni kuambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI na kisha ni kifo. Unajua ndugu mtafiti, wanaume siku zote wanaona na kutamani, na wanapotamani huomba, na kisha hukubaliwa.

Mawazo ya mtafitiwa huyu bado yanaonesha kwamba, mwanamke ndiye chanzo cha kumtamanisha mwanaume na kisha mwanaume kumhitaji kimwili. Kwa mantiki hii mwanamke ndiye Malaya na mwanamme ni mtakatifu. Hata hivyo, utakatifu wake una mashaka kwa sababu hata yeye anashiriki katika zinaa pamoja na mwanamke pia. Kwa upande wa jamii, wao hawatazami hali hii kwa mtazamo tulioutumia sisi na hivi ndiyo masuala ya Kijinsia yanavyotazamwa katika jamii mbalimbali za Waafrika.

Wataalamu wa nadharia ya ufeministi ambao kwao huhitaji usawa baina ya mwanamke na mwanaume wanapinga vikali dhana ya kumuona mwanamke tu ndiye Malaya bali hata mwanaume anayeshiriki katika masuala hayo naye pia ni Malaya

(Omary, 2010). Masuala ya msingi yanayoibuka hapa ni kwamba, mbona katika karne nyingi zilizopita wanawake na wanaume walivaa aina ya mavazi ambayo ilionesha sehemu ya miili yao na hakuna aliyemtamani mwanamke kwa sababu hiyo. Inakuwaje leo haya yanatokea hali ya kuwa hata hizo nguo zinazovaliwa na wanawake hazioneshi maungo yao kama ilivyokuwa huko nyuma. Hivyo basi, kwa maoni yetu, kusema kwamba, mwanamke anamtamanisha mwanaume na ndiyo maana mwanamke anakuwa malaya hakuna ukweli wowote bali ni masuala ya mfumo dume yaliyopo katika jamii ndiyo yanasababisha hali hii kuwa kama ilivyo.

5.1.3 Mwanamke Kiumbe Anayedanganywa Kirahisi

Mtazamo huu juu ya mwanamke umeenea katika jamii ya Watanzania kwamba, mwanamke ni kiumbe anayedanganyika kwa urahisi sana. Inaaminika kwamba, mwanamke hata awe na uwezo wa kumiliki kila kitu ambacho mwanadamu anastahili kukimiliki bado anaweza kudanganyika kwa vitu vidogovidogo na kisha kuushusha hadhi utu wake. Mtazamo huu unasawiriwa vizuri katika mashairi ya bongo fleva na washairi mbalimbali. King Crazy GK kupitia wimbo wake wa *Sista sista* anasema:

> Baba na mama yake walimpenda tena sana tu
> Na walimpa kila alichokitaka
> Ili walimwengu wasije kumuhadaa
> Na kama fedha walimpa nyingi
> Chakula kizuri kwa wingi
> Na hata mavazi mazuri kwa wingi
> Lakini bado yeye hakuridhika kwa magari
> Akababaika na vitu vidogo akachuuzika.

Dondoo hili linatoa taswira mbalimbali kuhusu mwanamke alivyokuwa ni kiumbe anayedanganyika kirahisi hata kama amepatiwa kila kitu na walezi wake. Msanii

anataja vitu kama fedha, chakula, mavazi na magari kuwa ni miongoni mwa vitu vinavyopendwa sana na wanadamu walio wengi lakini hasa mwanamke. Hata hivyo, vitu hivi mwanamke huyo aliyeitwa kwa jina la *sista* alipatiwa na wazazi wake ili asije akahadaiwa na walimwengu yaani wanaume. Pamoja na kupatiwa vitu vyote hivi bado hakuridhika na kisha akakubali kuhadaiwa na walimwengu na hatimaye akaupata ugonjwa wa UKIMWI.

Kimsingi, mawazo hayo hapo juu yanatoa taswira kwamba, mwanamke ana udhaifu fulani katika akili yake kiasi kwamba, akidanganywa huamini kaambiwa ukweli na akiambiwa ukweli huamini kadanganywa. Tunasema hivi kwa sababu kila hitajio muhimu la maisha kwa binadamu pamoja na ziada yake, huyu mwanamke alikuwa nayo sasa, iweje adanganywa kwa vitu vidogo vidogo? Bila shaka atakuwa na tatizo fulani la kiakili ama anaweza kuwa ni limbukeni. Hivi ndivyo namna wanawake wanavyo danganywa na walimwengu na kuonekana wao ni watu wa kudanganyika kirahisi rahisi tu. Nilipofanya mazungumzo/usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Manzese Dar es Salaam alinieleza kwamba:

> Mwanamke hata awe na kisomo cha juu na madigirii mengi kiasi gani bado atadanganywa tu na ataingia mkenge. Wapo akina mama ambao ni wasomi ambao mimi ninawajua lakini wanadanganywa na vijana wadogo tena wahuni tu hapa Manzese na kujikuta wanaharibu maisha yao hivi hivi.

Mawazo yaliyopo katika dondoo hapo juu yanasadidia hoja kwamba, mwanamke ni kiumbe anayedanganyika kwa urahisi na siku zote anapodenganywa huishia kupata madhara mbalimbali.

Msanii King Creyz (GK) anasema kwamba, daima mwanamke anapokubali kudanganywa basi huishia majuto ni mjukuu. Wale waliomdanganya hukaa pembeni na kuanza kumcheka kwa kuyakubali yale waliyomdanganya kwayo pasipo kumpatia msaada wa aina yoyote. Msanii anasema:

> Na safari hii Crayz (GK)
> Siyo kama naimba
> Bali nalia
> Nam
> Sista mwili akaweka rehani,
> Ikabidi akachange *Lifestyle*
> akaishi maisha ya kuchuna
> mabuzi
> Ilimradi fedha apate watoto cha kuwalisha
> Akawa anatisha umalaya
> Sister akafanya ndiyo kazi
> Mitaani akawa simulizi
> Akawa anakula vichwa kama
> Kinyozi
> Oh! Sista

Dondoo hili linaonesha kwamba, mwanamke anapokubali kudanganywa huishia kuishi maisha ya taabu na kisha kuingia katika ukahaba na umalaya. Dhana ile ya mwanamke ni Malaya inajitokeza tena katika wimbo huu. Wanaume wanaofanya nao huo umalaya hawatajwi kuwa nao ni waovu bali mwanamke peke yake ndiye muovu. Katika kusisitiza hilo msanii anaeleza kwamba, mwanamke huyu alifanya umalaya kuwa ndiyo kazi yake na *akawa anakula vichwa kama kinyozi*. Hapa msanii anatumia tashibiha kushadidia hoja yake kwamba, mwanamke huyu alikuwa anatembea/anafanya uzinifu na wanaume wengi kupita kifani. Kinyozi anaweza kanyoa hata watu zaidi ya kumi kwa siku moja kutegemeana na idadi ya wateja. Kama hivyo ndivyo basi mwanamke huyu aliyetajwa kwa jina la *sista* alitembea na wanaume zaidi ya kumi kwa siku hiyo moja. Hata hivyo, bado hailezwi hao wanaume walioliwa vichwa kama kinyozi nao ni malaya au la. Jambo la kusikitisha

na kushangaza ni pale tunapoelezwa kwamba, miongoni mwa waliomcheka binti huyu baada ya kupata matatizo aliyoyapata ni pamoja na wale waliomdanganya ambao ni wanaume. Anasema:

> Waliodanganywa wamemkimbia,
> Pembeni wamesimama
> Wangali mpenzi wanamcheka,
> Wanamuita Malaya
> Je, ungelikuwa wewe ungelifanya nini?
> Grazy GK, John Mahundi and Papaloving

Katika dondoo hili tunapata taswira kwamba, wanaume waliomdanganya binti huyu na kisha kumzalisha watoto na hatimaye kumuacha solemba ndiyo walewale wanaomcheka. Bila shaka hapa inaoneshwa kwamba, mwanaume naye ni kiumbe laghai kwa wanawake. Anamdanganya mwanamke kwamba, tufanye hivi na hivi halafu mimi na wewe tutaishi maisha mazuri pamoja na watoto wetu. Baada ya kukubaliwa watoto kupatikana mwanaume huyo humkimbia mwanamke na kumuachia watoto akiteseka nao katika kuwatafutia maisha. Katika kuonesha kwamba, mwanaume ni kiumbe katili kwa mwanamke msanii katika msitari wa mwisho wa dondoo tulilodondoa anasema anataja majina ya wanaume kuwauliza kama ingelikuwa ni wao (wanaume) ndiyo wamefanyiwa hivyo ingekuwaje? Hapa, msanii anawataka wanaume wanaohadaa wanawake wajiweke wao katika nafasi hiyo ya kudanganywa na kisha watendewe kama wanavyowatendea wanawake. Bila shaka wasingependa kujiweka katika nafasi hiyo na hivyo nao basi wasiwatendee wanawake hivyo wanavyowatendea na kuwadhalilisha. Haya ndiyo masuala ya kijinsia yanayoelezwa na kusawiriwa na wasanii wa bongo fleva katika mashairi yao.

Si hivyo tu bali pia, katika kuonesha kwamba, kudanganywa kwa mwanamke hakuna mwisho, yaani hapati fundisho kutokana na athari alizopata baada ya kudanganywa kwa mara ya kwanza msanii anasema:

> Akajiona amepunch mapenzi,
> Mashine akatega tena
> Ni watoto watano sasa anao na
> UKIMWI juu ameambulia
> Oh! Sista

Msanii anatumia sitiari *Mashine akatega tena* kumaanisha kwamba, amekubali kudanganywa kwa mara nyingine tena na kubebeshwa mimba iliyomfanya kuwa na idadi ya watoto watano ambao haelewi atawalea namna gani kwa kuwa hana uwezo wa kipato cha kumuwezesha kuwalea watoto hao katika maisha yaliyokuwa bora. Hata hivyo, hakuongezewa tu idadi ya watoto bali pia alizawadiwa ugonjwa wa UKIMWI. Baada ya kuzawadiwa ugonjwa wa UKIMWI ni dhahiri kwamba, maisha ya watoto watano alionao yatakuwa mashakani kwa sababu watabaki yatima baada ya mama yao kufariki dunia kwa kuwa mpaka sasa ugonjwa huu hauna tiba na hatima yake ni kifo kwa muathirika tena baada ya kupata mateso makubwa. Miongoni mwa mateso hayo ni haya yanayosemwa na msanii kuwa,

> Mwili umepukutika
> Nayo madonda yamemtoka,
> Masikini ameikanyaga miwaya
> Na sasa kitandani anawayawaya
>
> Amekosa msaada
> Mauti sista yamekwisha mkuta
> Angalia watoto wake aliowazaa
> bado ni wadogo sana
> Na still mama yao wanamuhitaji
> Na zaidi ya yote ye ndo
> baba ye ndo mama

Dondoo hili linatoa msisitizo tu wa yale tuliyoyaeleza hapo awali kuhusiana na mateso anayapata binti mtajwa kwa jina la *Sista* baada ya kuupata Ugonjwa wa UKIMWI. Vile vile, dondoo hili linashadidia hoja kwamba, watoto watano wa mama huyu hawatapata mtu wa kuwalea tena kwa kuwa mama yao alikuwa ndiyo baba ndiyo mama kwao. Hivyo kuondoka kwake duniani ni sawa na kusema kwamba, watakosa mtu wa kuwalea na hivyo maisha yao kuwa mashakani.

5.1.4 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe

Dhamira ya mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume ni dhamira kongwe katika ulimwengu wa fasihi. Momanyi (2000) anaeleza kwamba, mwanamke amesawiriwa kama chombo cha starehe kwa mwanaume katika kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili ukiwemo ushairi wa Shaaban Robert. Anaendelea kueleza kwamba, mwanamke anachukuliwa kama yai ambalo linatunzwa vizuri ili lisipasuke na wakati mwingine anakaa ndani kwa maana ya kurundikwa kama tunda ili liive vizuri tayari kwa kuliwa kwa maana ya kumfurahisha mwanaume. Washairi wa bongo fleva nao hawako nyuma katika kumsawiri mwanamke kama chombo cha starehe hasa kumstarehesha mwanaume. Msanii Ferooz katika wimbo wake wa starehe aliomshirikisha Prof. Jay, anasema:

> Saa saba juu ya alama saa
> Nikiitazama
> Nimeshaaachana na Jack sasa
> namfuata Salama
> saa kumi na mbili ninaapoittment
> na mademu wawili
> achana na yaule ambaye tutakutana saa mbili,
> Mgeni wa Mikocheni ambaye

hayupo tena duniani
alikuwa akinisubiri pale maskani
kijiweni

Amina anasema tutakutana kwa
macheni
na kila siku tu najirusha
tena kwa foleni
Huo ndio ulikuwa mwenendo
wa maisha yangu,

Mimi kujivinjari na machungu
starehe nilizifanyia papala nibadili
mademu kama vidaladala
nikienda nimepanda hili
nikirudi nimepanda lile.

Dondoo hili linatoa taswira mbalimbali kuashiria kwamba, mwanamke anaonekana kama ni chombo cha starehe kwa mwanaume katika jamii. Hili linaonekana pale ambapo bwana Ferooz anapokutana na kufanya tendo la ndoa na wanawake kama akina Jack, Salama, Mademu wengine wawili, Mgeni, pamoja na Amina kwa siku moja. Kwa msingi huu, mwanamke anaonekana kama chombo cha kumstarehesha mwanaume kama sio kumstarehesha basi mwanamke mmoja tu angemtosha kukidhi haja zake, kwa nini wote hawa?

Katika kuonesha msisitizo kwamba, mwanamke ni chombo cha starehe, msanii anatumia tashibiha kushadidia hoja zake. Anasema: *Starehe nilizifanyia papala, nilibadili mademu kama vidaladala*": Daladala hupandwa na watu kisha huteremka kila kituo na wengine huingia kisha tena hushuka na kuwa ndio mtindo huo kila siku iendayo kwa Mungu. Hapa mwanamke anafananishwa sawa na daladala ipandwayo na kila mtu. Kwa msingi huo basi, mwanamke ni chombo cha kuwastarehesha

wanaume katika maisha yao ya kila siku. Nilipofanya usaili na mtafitiwa mmoja kuhusiana na hali hii alinieleza kwamba:

> Ndugu mtafiti, wanawake wanachukuliwa kama viumbe walioumbwa kumburudisha na kumstarehesha mwanaume. Kimsingi, jambo hili linaonekana hata katika vitabu vya dini ambapo tunaona wanaume wameruhusiwa kuoa hata wanawake wanne na kuwafanya wote kuwa wake zake.

Tutazamapo mawazo yanayowasilishwa katika hili kwa makini tunapata uelewa kwamba, jamii ina mtazamo kuwa mwanamke ni chombo kilichoumbwa kwa minajili ya kumstarehesha mwanamme ndiyo maana hata mtafitiwa huyu anajaribu kuhalalisha mtazamo wake kwa kutumia vitabu vya dini. Hata hivyo, maandiko katika vitabu vya dini hayaruhusu mwanaumme kuoa mwanamke zaidi ya mmoja kwa minajili ya kumstarehesha mwanaumme huyo bali kwa sababu mbalimbali zenye hekima ndani yake, ambazo hatuwezi kuzieleza hapa kwa kuwa si sehemu ya madhumuni ya utafiti huu.

Tukiachilia mbali usawiri wa mwanamke ulioelezwa katika dondoo kutoka kwa msanii Ferooz tunaona pia hata mwanaume kwa upande mwingine naye amesawiriwa kama kiumbe mpenda starehe. Ni kiumbe mpenda starehe kwa sababu amekuwa akiwabadilisha wanawake kama daladala kwa maana ya kwamba, leo yuko na huyu kesho yuko na yule na kadhalika. Hata hivyo, kwa upande wa jamii mwanaume huyu haonekani kuwa ni mkosaji kwa kiwango kile kile cha mwanamke bali kwa kufanya hivyo huonekana yeye ndiye kidume cha mbegu katika jamii. Mambo haya hujidhihirisha pale ambapo baadhi ya wanaume hujisifu mbele ya wanaume wenzao kwamba, wao wana wanawake wengi na hivyo kujionea fahari. Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba, mwanamke anachukuliwa kama chombo cha

starehe kwa mwanaume katika jamii basi na mwanaume achukuliwe kama kiumbe ama chombo cha kupenda starehe. Hili linathibitishwa na mawazo ya Feroozi pale anaposema:

> Nilitamani starehe zote nizitawale
> Hata kumkumbuka mola ilikuwa ndoto
> Nilitekwa na ulimwengu kumbe naukimbilia
> moto
> katika kubadili wasichana
> nilikubuhu, nilitembea na
> Watoto wa geti, machangu na
> masista duh
> Ubaya kwamba kondomu sikuitambua
> Kwa kujua kwamba ladha ya
> mapenzi itapungua
> kumbe nilikuwa napotea njia
> Niliyoshauriwa mimi niliyapuuzia.

Msanii anashadidia hoja yetu ya msingi kwamba, mwanaume ni kiumbe mpenda starehe kwa kutaka kuzitawala aina zote za starehe zinazopatikana duniani hasa ile ya kujamiiana na wanawake wa kila aina. Anasema kwamba, alitembea na *watoto* hapa anatumia sitiari, kwama wasichana waliokuwa wakifungiwa ndani, machangudoa na wale waliojinata na kujisikia (masista duh) wote hawa alitembea nao tena bila kutumia kinga (kondomu). Msanii anasema kwamba: “hakutumia kinga kwa kuhofia kupunguza ladha ya mapenzi.” Hii yote inaonesha ni namna gani mwanaume anachorwa kama kiumbe mpenda starehe.

Msanii anaonesha msisitizo kwamba, starehe hasa ndizo zinazowaponza watu wengi na kisha kuzima nyota za maisha yao kama mshumaa uzimikapo pale unapopitiwa na upepo anasema kwamba:

Hapa nilipo mimi nipo kitandani,
Starehe zimeniweka matatani,
Kupona tena haiwezekani,
Masela wangu ndugu zangu
Buriani
Kwaherini, Kwaherini, Kwaherini.

Dondoo hili linaonesha kwamba, mwanaume ni kiumbe mpenda starehe na sasa starehe hizohizo zimemuweka matatani kwa maana kwamba, zimefanya kupata ugonjwa wa UKIMWI ambao hatma yake ni kifo. Kwa namna ile ile ya kawaida ya binadamu anaonesha kwamba, binadamu hujuta baada ya tukio kutokea lakini Waswahili walisema, majuto ni Mjukuu.

5.1.5 Sifa na Mapambo kwa Mwanamke

Hapo awali tumeeleza usawiri wa mwanamke na hata mwanaume kwa namna mbalimbali. Kwa mfano: tumeona mwanamke kama kiumbe duni asiyeweza kufikiri na kupanga juu ya maisha yake, mwanamke kama kiumbe wa kudanganywadanganywa tu na wanaume na mwanamke kama chombo cha starehe sasa tuangalie namna mwanamke anavyopambwa kwa sifa mbalimbali na mwanaume. Msanii Dully Sykes akiwashirikisha Joselin na Blue anamsifu mwanamke kwa sifa kemkemu kuwa:

Nakupenda maa! Basi njoo maa!
Nikila saa kabisa! Uko kwa kichaa!
Girl just listen, tuishi kama heaven
Nakuweka kwenye top 10
Nadata na *reception*
Mi nachoka hai, pande zote
huniboi

Niite baby boy to me, achana
Na toy

Dozz pipo doz mapozi
Sasa dozi na hisia za machozi
Na napenda zako nywele ndefu
Zimekwenda shule, upande wa
maumbile

Nadata toka pande ile
Sura yenye mvuto mashavu
yenye dimpose x 2

Msanii anatumia sitiari za aina mbalimbali katika kumpamba na kumsifia mchumba wake. Kwanza, anasema kwamba anadata na reception kwa maana ya anavutiwa sana na mwonekano wa huyo mchumba wake. Reception ni sehemu ya mapokezi katika hoteli ama kumbi, benki na kadhalika ambapo sehemu hii huwa mbele na ndiyo ya kwanza kuonekana pale tu mgeni ama mteja anapoingia. Hivyo basi sehemu hii huwa ni safi muda wote ili kuwavutia wateja na kisha kupenda huduma zitolewazo katika sehemu hiyo. Vinginevyo kama mapokezi ni sehemu chafu basi wateja huamini kwamba mandhari nzima ya sehemu hiyo nayo ni chafu na hivyo kutoipenda sehemu hivyo. Kwa ufupi binti huyu anayesifiwa hapa anaonekana ni mtanashati na mrembo kwelikweli kwa kuwa *reception* yake ni nzuri.

Msanii hakuishia hapo tu bali anaendelea kusifu nywele za binti huyo kwamba, ni ndefu na *zimekwenda shule*. Sitiari *zimekwenda shule*, inaonesha msisitizo kwamba, ni nywele nzuri sana tena zenye kuvutia. *Shule* ni mahali ambapo wanajamii/watoto hupatiwa maarifa ambayo yatawaongoza katika maisha yao ya kila siku. *Shule* ni mahali pa kufuta ujinga na kumpa mwanafunzi maarifa na weledi. Sasa nywele kusifiwa kwamba zimekwenda shule bila shaka ni nzuri sana na zinampendeza binti huyo na kuwavutia wote wanaozitazama. Katika kiitikio tunaelezwa kwamba binti huyo ana sura ya kuvutia na mashavu yenye *dimpose*. Hapa msanii anamaanisha

kwamba, binti huyo ana sura nzuri sana na anapocheka ama kutabasamu basi mashavu yake hubonyea.

Msanii hakuishia hapo bali ameendelea kumsifu mchumba wake huyo kwa kumfananisha na dhahabu. Anasema:

> "Oh! oh! oh! Yaani soo!
> Nimepata *dhahabu* mtoto wa Kariako
> *Mtoto* anavutia upande ooh!
> *Mtoto* anakomesha mpaka
> Mabishoo x 2

Kwa hakika dhahabu ni kito cha thamani kubwa sana na huvutia macho kukitazama kwa uzuri wake. Hivyo thamani na uzuri wa dhahabu unafanisha na binti huyo anayesifiwa na msanii. Vile vile, msanii anamwita binti huyo kuwa ni "mtoto". Hii ni sitiari inayoashiria kwamba, binti huyo ni mzuri sana kiasi cha kufananishwa na mtoto mdogo aliyezaliwa. Mtoto mdogo anapozaliwa, watu wengi humwita malaika kutokana na uzuri wake. Pia mtoto mdogo huwa anapendwa sana na wazazi wake na huhakikisha kwamba, anapata ulinzi na kila kitu anachokihitaji. Sifa zote hizi anapewa binti huyu ambaye ni mchumba wa msanii.

Baada ya maelezo marefu kuhusu sifa alizotumia msanii kumpamba mchumba wake sasa tujadili masuala ya kujisia yanayosawiriwa katika madondoo yaliyo wasilishwa kwetu na msanii huyu. Kwanza, mwanamke anasawiriwa kama kiumbe mzuri asiye na kifani na kwa hali hiyo kumvutia kila anayemuona. Kinachoelezwa hapa ni kwamba, wanaume wanapenda sana umiliki wa vitu yaani mali na wanawake pia na daima hupenda vile ambavyo ni vizuri. Mwanaume hapendi kusubiri watu wengine wamsifie mke ama mchumba wake bali yeye mwenyewe huanza kumsifia kwanza.

Hivyo, hupenda kutoa sifa za mke wake kwa rafiki zake, ndugu, jamaa na marafiki ili waone kwamba anaye mwanamke ama mchumba mzuri kuliko wanawake wote duniani. Kwa upande mwingine wanawake nao hufurahi sana pale wanaposifiwa na kujiona kwamba wako katika daraja ya juu mno miongoni mwa daraja za maisha ya mwanadamu. Mwanamke anaposifiwa basi huwa tayari kumridhisha yule anayemsifia kwa namna yoyote ile. Kama hivyo ndivyo, ndio maana watu wengi hasa wanaume hutafuta sitiari nzito nzito za kuwasifu wanawake ili waone kwamba wanapendwa sana na kisha wawakubalie wanaume hao (wanaowasifu) kuwa wenza wao.

Masuala mengine ya kijinsia yanayotokeza katika madondoo ya msanii hapo juu ni kwamba: Vijana wengi wa kiume wanapofikia hatua ya utu uzima hupenda sana kuzungumzia masuala yanayohusiana na mahusiano baina ya mwanaume na mwanamke katika kufanya hivyo humakinikia sana katika kumsifu mwanamke. Hali hii imeenea katika nyimbo nyingi za muziki wa bongo fleva na kufanywa karibu asilimia 990 ya nyimbo hizo kuwa zinazungumzia masuala ya mapenzi. Akitoa maoni yake kuhusu ukweli wa hali hii Mulokozi (2010 katika tamasha la elimika na bongo fleva) anasema:

> Msiwashutumu vijana kwa kuzungumzia masuala ya mapenzi katika nyimbo zao za bongo fleva. Ninasema hivi kwa sababu kuwakataza kuzungumzia masuala hayo ni kuwanyima haki yao ya msingi kwani kwa umri walionao ndio muda muafaka wa kuzungumzia mambo hayo au mnataka wazungumzie masuala hayo wakiwa wazee?

Tunakubaliana kwa asilimia mia kwa mia na mawazo ya Mulokozi (ameshatajwa) kwamba, ni katika umri wa ujana ndipo hasa vijana huzungumza masuala ya

mapenzi kuliko wakati wa uzee kwa kuwa ujana ni maji ya moto. Kama hivyo ndivyo basi vijana hutafuta sitiari za aina mbalimbali kuelezea masuala ya mapenzi likiwemo hilo la kuwasifu wale wanaowapenda. Hata hivyo, wasanii wa kiume wanaonekana kuwasifu zaidi wanawake kuliko wanawake kuwasifu wanaume ingawa wako wachache wanaofanya hivyo.

Msanii katika wimbo huu anaendelea kueleza kwamba, naye (msanii) alisifiwa na binti huyo ingawa sifa zake si sawa na zile alizozitoa yeye kwa binti huyo. Msanii anasifiwa kuwa anajua kuimba vizuri na tena anajua kuipangilia mistari ya mashairi yake vizuri, mpaka huyu binti *anazimika* kwa hilo. *Kuzimika* hapa limetumika kuonesha kwamba, binti anafurahishwa na huyu anayeimba kiasi cha kukosa kifani. Si tu kuzimika bali pia *anamfagilia* msanii kwa uimbaji wake mzuri. Hapa tunaoneshwa utofauti wa uteuzi wa sitiari anazotumia mwanaume kumsifu mwanamke na zile anazotumia mwanamke kumsifu nazo mwanaume. Kwa ufupi mwaume anasifiwa kwa kazi yake na mwanamke anasifiwa kwa umbo sura na kwa ujumla mwili wake.

Msanii Dudu baya naye katika wimbo wake wa *mpenzi* anamsifu mchumba wake kwa sifa nyingi na nzuri. Anasema:

> Wewe mjanja si *mpolipoli*
> *Nimezimika* nimekufa nimeoza
> Shingo yako town ni *mkonga*
> Midomo yako taiti kimanzi
> Nimedata nawe *waridi*
> Nakusifu wangu we kipenzi.

Hapa msanii anamsifu mpenzi wake kwa kutumia viungo vyake vya mwili kama vile shingo inafananishwa na mkonga, midomo yake ni mizuri sana kwa kufanya

“romance” na kadhalika. Kwa msingi huu, hatofautiani na Dully Sykes kama tulivyoona hapo awali. Vile vile, anamsifu mpenzi wake kwa kumfananisha na *Ua* aina ya Waridi ambalo ni ua zuri sana kwa muonekano linang’aa na linatoa harufu nzuri sana ya kuvutia. Hivi ndivyo namna mwanamke anavyosawiriwa kupitia mashairi ya muziki wa gongo fleva.

Msanii Dudu baya anaendelea kuonesha kwamba, mwanamke ni kiumbe anayepaswa kutunzwa ili wakati wote aonekane anapendeza na mwenye mvuto kwa jamii. Anayasema haya pale anaposema:

> Usivyoringa na wako uzuri najua unaelewa
> wengi wao hawaelewi x 2
> Mwanamke ni sawa na *gari* kupata
> service kila mara kubeba mizigo sawa
> na tairi likizidisha linachoka kongoroka x 2
> Mwanamke kuzidisha wanaume ni lazima
> achoke akongoroke wanaume nao toweka
> Chomeka mzizi.

Kauli ya Dudu baya kwamba, mwanamke ni sawa na gari inaonesha kwamba, mwanamke anatakiwa kupatiwa matunzo ya kutosha ili daima aendelee kupendeza na kuvutia machoni pa watazamaji. Hii yoyote inaonesha namna mwanamke anavyosifiwa na kupendwa na mwanaume kupita kiasi.

5.1.6 Mwanaume Kupendwa na Mwanamke

Suala la mwanamke kumpenda mwanaume ni suala la kawaida katika jamii. Ila si jambo la kawaida mwanamke kumtamkia mwanaume waziwazi kwamba, anampenda tena pale wanapokutana kwa mara ya kwanza. Mara nyingi mwanaume ndiyo huanza kumweleza mwanamke kuwa ninakupenda na mwanamke naye hurudishia kwa

kujibu nami nakupenda kama amekubaliana. Msanii Prof. Jay kupitia wimbo wake wa *Zali la Mentali* anabainisha kwamba hata wanawake nao siku hizi huwatamkia wanaume kwamba anampenda na tena mwanamke kutoka katika familia tajiri anamtamkia mwanaume kutoka familia masikini tena hohehahe. Msanii anasema:

> Naitwa Vick nina miaka 22 ni mtoto
> wa kipekee kwenye familia ya kitajiri
> Oh naitwa Jay ukiniita fukara haukosei
> Na naishi kwa nguvu za macho siku
> zenyewe hazisogei
> Alishuka toka garini
> na kusema
> “Jay nakupenda”.

Msanii anaeleza kwamba, la suala mapenzi kwamba hayachagui lina ukweli ndani yake. Hii inatokana na ukweli kwamba, mwanamke anayetokea katika familia ya kitajiri anampenda na kumtamkia kijana masikini hohehahe kabisa. Huu ndio ukweli kuhusu maisha kwani mambo haya yapo katika jamii na yanatokea na kutendeka kila uchao. Ingawa mapenzi yanahusishwa na masuala ya umiliki wa mali na fedha ila hapa tunaona mambo ni tofauti kabisa. Inavyofahamika ni kwamba, wasichana wengi hudanganyika kwa fedha na mali alizonazo mwanaume na kisha kukubali kuwa nae kimapenzi. Lakini kwa Vicky hali ni tofauti kabisa. Yeye ni tajiri na Jay ni masikini Lakini Vicky amempenda Jay na kumtaka awe mpenzi wake.

Dondoo hilo hapo juu linaonesha kwamba, Jay alishangaa kusikia maneno yaliyokuwa yakitamkwa na Vick akilinganisha na hali yake ya maisha. Kuonesha msisitizo huo Jay anatumia sitiari kwamba, yeye anaishi kwa *nguvu za macho*. Sitiari hii inaonesha kwamba Jay hana kitu chochote zaidi ya mwili wake na mkokoteni anaoutumia katika kujitafutia riziki. Hata hivyo, pamoja na umasikini wake bado

alikubaliwa na kupendwa kimapenzi na Vicky jambo ambalo kwa hali ya kawaida halitegemewi kutokea. Baada ya muda kupita, Jay na Vick walifunga ndoa na kuishi kama mke na mume. Msanii anasema:

> Ilifika siku ya siku mentali Jay ndani ya jumba na
> Vicky ndani ya shela hakuna uchawi wala ndumba.
> Tulishikana mikono ni nderemo na vifijo
> *Tukafunga pingu za maisha* kanisani bila fujo.

Msisitizo juu ya ndoa yao unaelezwa kwa kutumia sitiari *tukafunga pingu za maisha*. Hivi ndio namna Jay na Vicky walivyokamilisha safari yao ya maisha ya kupendana.

Kimsingi, ni jambo lililozoeleka katika jamii kuona tabaka tajiri kutopenda mmoja wa wanafamilia wao anaoa au kuelewana na mtu kutoka tabaka la watu masikini. Hata hivyo, nguvu ya mapenzi wakati mwingine hushinda mipaka ya kitabaka na wawili wapendanao kuoana na wazazi nao kuungana nao na kuwasaidia katika kusukuma mbele mapenzi yao. Haya tunayapata pale Jay anaposema:

> Zawadi zilizagaa zilikuwa nyingi tena kemkem
> Baba mkwe alitupa benzi, kiwanda, nyumba na BM.
> Acha zawadi nyingi kutoka kila sehemu.

Dondoo hili linathibitisha kwamba, wazazi wa Vicky ambao walikuwa ni matajiri wakubwa walimkubali Prof. Jay kumuoa binti yao na kisha kuwapatia zawadi za aina mbalimbali ili waishi maisha ya raha mustarehe. Hii yote imesababishwa na nguvu ya mapenzi aliyokuwa nayo Vicky kwa Prof. Jay.

5.1.7 Wanawake na Mapenzi ya Pesa

Katika sehemu iliyopita hapo juu tumeona mwanamke ambaye ni tajiri amempenda mwanaume ambaye ni masikini tena hohehahe. Kwa upande mwingie wapo

wanawake ambao hupenda kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume ambao wana uwezo wa mali na fedha. Wanawake wa aina hii kamwe hawapendi kuwa na uhusiano na wanaume masikini. Haya yanathibitishwa na maneno ya Prof. Jay pale anaposema:

> Nilikumbuka nikacheka nilivyoteswa na wale mademu.
> Mambo swadakta nipo na Vick
> Kidume nang'aa wanajigonga shenzi taipe (shenzi type)
> Nilipokuwa *arosto* mlinikwepa *kama ukoma*
> Mambo juu ya msitari kunisalimu mnaona *noma*.

Dondoo hili linaanza kwa kueleza kwamba, *niliteswa na wale mademu* ambayo ni sitiari inayoashiria wasichana waliomkataa Prof. Jay kwa sababu hakuwa na chochote kuhusiana na fedha na mali nyinginezo. Hii inaonesha kwamba, wasichana hawa hawakuwa na mapenzi ya dhati bali mapenzi ya fedha kwa Prof. Jay ambaye alikuwa ni masikini wa kutupa. Katika kuonesha msisitizo kwamba, alikataliwa na wasichana hao kutokana na ukata uliokuwa unamkabili anasema nilipokuwa arosto mlinikwepa *kama ukoma*. Msanii anatumia tashibiha hii kuonesha namna mtu masikini anavyokosa thamani mbele ya wasichana wanaompenda mwanaume kutokana na uwezo wake wa kifedha. *Ukoma* ni ugonjwa unahusisha kukatika vidole vya mikono na miguu kwa muatirika na ugonjwa huu huambukizwa kwa kushikana mikono na waadhirika wa ukoma. Hivyo, watu huogopa sana ugonjwa huo ili wasije kuambukizwa. Hii inaonekana hata pale waathirika wa ugonjwa huo wanaomba msaada wa fedha barabarani hutumia chombo kama kikombe kwa ajili ya kuwekewa fedha na wale watakaopenda kuwasaidia. Hii yote ni kwa ajili ya kuzuia kushikana mikono ili watoa msaada wasiambukizwe ugonjwa wa ukoma.

Katika sehemu nyingine msanii anaonesha kwamba, wasichana na wanaopenda wanaume wenye fedha hawapendi kuongea na wanaume masikini. Wakati mwingine hata wakiulizwa maswali fulani hata baada ya kuombwa samahani na mwanaume masikini huwa hawapendi na kuona kama wanashushwa hadhi yao, msanii anasema:

> …Nikaona toto ya nguvu nikajikuta nimeropoka
> "Dada habari samahani naomba niulize swali"
> Akajibu "Maskini koma tafadhali hii *ngoma ya gari*
> Dada mbona mkali, "wee" Kinyago kubali yaishe
> Ni kasema Inshala sawa hii yote kwa sababu ya fukara…

Dondoo hili linashadidi hoja kwamba, wapo wanawake ambao hawapendi kuwa na maongezi ama mazungumzo yanayoletelea kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanaume masikini na fukara. Kwa maana hiyo wao wanapenda kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanaume tajiri peke yake. Msanii anatumia sitiari hii *ngoma ya ngari* aikimaanisha ni mwanamke anayetoka na wanaume ambao wana uwezo wa kifedha na mali na hivyo hawezi hata kuzungumza na mwanaume masikini na fukara kama Prof Jay. Baada ya kuona namna mwanamke anavyosawiriwa kama mpenda mapenzi ya fedha ni vema sasa tuone namna mwanamke anavyosawiriwa kama mlezi katika jamii.

5.1.8 Mwanamke Mlezi wa Jamii/Familia

Dhamira ya mwanamke kama mlezi wa familia imekuzwa sana katika kazi mbalimbali za fasihi kama vile riwaya, tamthilia na ushairi na hata hadithi fupi pamoja na fasihi simulizi. Wasanii wa muziki wa bongo fleva nao hawako kando katika kuisawiri dhamira hii adhimu katika mashairii yao. Mama kama mlezi amekuwa akisawiriwa katika nyimbo za bongo fleva kwa kutumia taswira, sitiari

tashibiha na ishara mbalimbali ili kuonesha umuhimu wa nafasi ya mama katika malezi ya jamii. Msanii Banana Zorro ni miongoni mwa wasanii aliyewasilisha dhamira hii katika wimbo wake wa *Mama Yangu*. Katika wimbo huu msanii anaonesha kuwa ni mama, mlezi wa familia na anastahili kupongezwa na kuheshimiwa kwa hilo. Anasema:

> Mama yangu wewe ni nguzo maishani mwangu (mwangu)
> Ni *taa* imulikayo mbele (yangu) daima milele.
> Mama yangu wewe ni nguzo maishani mwangu (mwangu)
> Ni taa imulikayo mbele (yangu)
> mawazo yako mamaa yaniongoza maisha yangu yooo.

Tutazamapo mistari ya madondoo hayo hapo juu tunaona msanii anamfananisha mama na nguzo. Nguzo ni aina ya mti, ubao ama “cement” iliyosimikwa ardhini kwa ajili ya kushikilia vitu kama vile paa la nyumba, ghorofa na kadhalika pasipo kuwepo kwa nguzo hizo basi paa ama ghorofa hilo haliwezi kuimarika kama inavyopasa na badala yake litaanguka. Kwa upande wa dini ya Kiislamu kwa mfano tunaelezwa kwamba, uislamu umejengwa juu ya nguzo tano ambapo iwapo mtu/muumini hatatekeleza nguzo hizo kwa ukamilifu basi kamwe hawezi kuwa mwislamu kamili. Kwa msingi huu, nguzo ni kitu cha muhimu sana. Msanii hapa anatueleza kwamba, mama ndiye anayetoa mustakabali wa maisha ya mwanawe pale anapokuwa mtu mzima. Iwapo mama hatatoa mafunzo na malezi yapasayo kwa mtoto wake basi mtoto huyo ataishi maisha ya taabu kwa maana ya kukosa nidhamu, uvumilivu upendo uchapakazi na kadhalika.

Vilevile, msanii anasema mama ni *taa* imulikavyo maisha yake. Hii ni sitiari inayoonesha kwamba, mtoto huongozwa na misingi aliyofunzwa na mama yake wakati akiwa mdogo mpaka anafikia katika utu uzima. *Taa* hutoa nuru pale palipo na

giza pakatapakaa mwanga na mama nae ni hivyo hivyo. Kwanza anamzaa mtoto kutokea kizani kwa maana mtoto huyo anakuwa hafahamu chochote katika ulimwengu. Baada ya hapo mama humpatia matunzo chakula (maziwa) na baadaye humfunza lipi zuri na lipi baya ambayo ndio msingi wa maisha ya mtoto ya baadaye na ndiyo taa hiyo anayoizungumzia msanii. Hili linashadidiwa na kauli ya msanii pale anaposema "mawazo yako mamaa yana miongozo maisha yangu yoyooote." Mawazo yanayosemwa hapa ni yale mafunzo mama anayompa mtoto wake tangu anazaliwa mpaka anakuwa mtu mzima.

Kimsingi, mama ana nafasi kubwa katika ulezi wa familia na mtoto kwa ujumla. Hii inatokana na ukweli kwamba mama ndiye hukaa na watoto katika muda mwingi wa maisha yake kuliko baba. Mama huanza kukaa na mtoto tangu akiwa tumboni mwake na baada ya kuzaliwa mtoto huwa mikononi mwa mama yake mpaka afikishapo umri wa miaka saba ndipo huanza kujitegemea na kuanza kuondoka mikononi mwa mama. Hata hivyo, mtoto huendelea kupata mafunzo na maelekezo juu ya maisha kutoka kwa mama yake mpaka pale anapoanzisha maisha ya kujitegemea/kuanzisha nae familia yake.

Msanii anaendea kueleza kwamba ingawa mama ana thamani kubwa isiyokifani lakini wapo baadhi ya wanajamii wanaoishusha thamani na hadhi ya mama katika jamii. Anasema:

> Mama ingawaje jamii inakushusha hadhi
> Kwangu nakubali tafadhali sioni
> Kwa nini mama miezi tisa uliyonibeba
> Siwezi kukulinganisha na hii *miba* unayonivusha
> Makosa mengi nakufanyia lakini unanikumbatia
> Cha kukulipa sikioni.

Msanii anatumia sitiari *nakukubali mama* kuonesha kwamba, mama ni mtu muhimu sana na hakuna anayeweza kumshusha hadhi akafanikiwa badala yake anaweza kupata radhi na kupata taabu katika maisha yake yote. Msanii anasema mama ni kiumbe wa ajabu sana hata umtendee makosa mengi kiasi gani bado yeye atakuonya na kisha kukusamehe na vigumu sana kumsusia mwanae. Hii ndiyo roho ya ulezi wa familia aliopewa mama ambapo ingekuwa vinginevyo basi hali a malezi ya familia ingekuwa taabu sana. Taifa lingekuwa na kizazi ambacho hakina malezi bora na hivyo hata kutawalika ingekuwa ni vigumu sana.

Si hivyo tu bali pia, msanii anasema kwamba, cha kumlipa mama kutokana na jinsi anavyoilea familia hakipo. Kazi anayofanya mama ikisemwa mtoto ailipe basi itamgharimu maisha yake yote bila kufanikiwa kumlipa mama. Hivyo, cha msingi anachopendekeza msanii ni kumpenda na kumeheshimu mama katika maisha yake yote na hiyo ndiyo zawadi pekee kwake katika kuthibitisha hili msanii anasema:

> Nikisema nikulipe itanigharimu maisha yangu yote.
> Nikisema nikuzawadie sioni kile unachostahili
> Ninachoweza sema nakupenda sana mama
> Ninakushuru kwa mema yote uliyotenda
> kwangu mama weweeee

Dondoo hili linashadidia hoja kwamba, kumlipa mama kwa ukarimu wake anaoutenda kwa mtoto na familia yake ni suala gumu sana na kamwe haliwezekani kuurahisi na halitakaa liwezekane. Malipo kwa mama kutokana na wema wake ni kufuatilia yale mazuri anayowafunza watoto wake na kuyatumia katika maisha yao ya kila siku. Hii ndiyo tunzo pekee kwa mama. Baada ya kuona namna mama alivyosawiriwa kama mlezi katika jamii sasa tuone mama anavyosawiriwa kama kiumbe jasiri na shujaa kupitia wimbo huu huu wa Banana Zorro.

5.1.9 Mama Kiumbe Shujaa na Jasiri

Dhamira ya ushujaa na ujasiri imejadiliwa sana katika tendi simulizi na andishi na mwanaume ndiye hasa anayetajwa kuwa shujaa na jasiri huku mwanamke akiachwa nyuma katika hili (Omary, 2011). Ushujaa wa mwanaume unahusishwa na kupigana na kushinda vita, kuzaliwa kwa njia na namna zisizo za kawaida, kuwa na nguvu nyingi pamoja na akili nyingi (Omary, 2010). Hata hivyo, mwanamke ambaye ndiye humzaa huyu shujaa tena kwa taabu nyingi yeye hatajwi popote kama naye ni shujaa. Wasanii wa bongo fleva akiwemo Banana Zorro anaonesha ushujaa wa mama pale anaposema:

> Ni tuzo gani unayostahili kwa kuweza oooh
> Kustahimili shida zangu ooh na usumbufu
> Wangu toka kuzaliwa kwangu mpaka leo
> Na siamini mbele yako
> Mama unastahili sifa
> Kwa mapenzi uliyoonyesha
> Kwangu tangu nazaliwa
> Mama yangu oooh oooh.

Dondoo hili linatoa taswira kwamba, mama anapata shida nyingi sana tangu pale anapobeba ujauzito, anapojifungua na baada ya kumlea mtoto. Usumbufu na shida hizi zinatosha kabisa kumfanya mama kuwa shujaa katika jamii. Wakati mama anapata shida hii wanaume walio wengi wanakuwa katika shughuli zao kama vile kunywa pombe, kucheza bao na shughuli nyingine zisizo na tija kwa familia na jamii kwa ujumla. Hata hivyo, bado mama ataonekana hajafanya kazi yoyote kubwa kwa sababu hakuingiza fedha kwa kufanya kazi ya ulezi wa mtoto na familia. Kwa maoni ya msanii, mama anastahili kuitwa jasiri kwa kuhimili adha na usumbufu mkubwa anaoupata katika malezi ya mtoto tangu akiwa tumboni mwake mpaka anamzaa na kisha kumlea.

Mawazo ya msanii Banana Zorro hayako mbali sana na wanazuoni wa masuala ya utendi kama vile Mulokozi, Mbele na wengine juu ya ushujaa wa mwanamke kutokana na shughuli zake ya ulezi wa jamii kwa ujumla. Wanataalimu hawa wameenda mbali na kueleza kwamba, Mwanakupona katika *Utenzi wa Mwanakupona* anastahili kabisa kuitwa shujaa kwa yale ambayo anatakiwa kuyatekeleza kwa mume na familia yake tangu anaamka mpaka analala usiku. Mambo anayofunzwa binti huyu na mama yake na kwamba ayatekeleze kwa mume wake ni mazito sana na utekelezaji wake unahitaji moyo wa ujasiri na ushupavu kabisa. Kwa hakika Mwanakupona anastahili kuitwa shujaa. Niliongea na mtafiti mmoja kutoka Dar es Salaam kuhusu ushujaa wa mwanamke, akanieleza kwamba:

> Kwa hakika kubeba mimba miezi tisa na kisha kumzaa mtoto halafu tena kumlea mpaka afikishe miaka mitatu tu ni kazi nzito sana na inahitaji ujasiri na ushupavu mkubwa. Wakati haya yote yanafanyika si kwamba, mama hafanyi shughuli nyingine la! Anaendelea kufanya shughuli nyingine nyingi. Anatakiwa amtunze mumewe, watoto wengine, ndugu, mawifi, mashemeji na marafiki kwa kuwapikia chakula na kuhakikisha vyombo ameosha nakadhalika. Wakati mwingine akichoka akashindwa kutofanya shughuli hizi basi hulaumiwa kwa hila lakini anapomudu shughuli zote hizi hapewi hata shukurani ya asante.

Mawazo haya kimsingi yanaonesha shughuli mbalimbali zinazofanywa na mama ambazo kwazo zinamfanya mama nae kuwa na sifa ya ushujaa na ujasiri katika jamii. Wananadharia ya ufeministi wanasema kwamba, mwanamke kufanya shughuli zote ni uonevu mkubwa na inarudisha nyuma maendeleo ya mwanamke (Omary, 2011) kwao, mwanamke anastahili kulipwa fidia kwa maana ya mshahara kama wanavyolipwa wale wafanyao kazi katika maofisi mbalimbali. Kwa kufanya hivyo mchango wa mwanamke utakuwa umetambuliwa na kuenziwa kwamba ni muhimu katika kulisukuma mbele gurudumu la maisha ya jamii na taifa kwa ujumla.

Kimsingi ni jambo lisilopingika kwamba mwanamke anatumia muda wake mwingi sana katika kumlea mtoto kuliko ilivyo kwa baba wa mtoto. Msanii Banana Zorro anathibitisha hili pale anaposema:

> Umenilea tangu ni zialiwe
> Haukuchoshwa na wangu usumbufu uu
> Muda wako mwingi mama ulintumia kwa ajili yangu
> Oooh asanteh mama unstahili sifa
> kwa mapenzi ulioonyesha tangu nazaliwa
> Mama yangu oooh, asanteh Sana mamaaa ooh.

Taswira inayotolewa katika dondoo hapo juu inaonesha kwamba, mama ni mtu anayekaa na mtoto kwa maana ya kumlea kwa miaka mingi huku akipata taabu na shida nyingi. Kwa msingi huu basi, mama anapaswa aheshimiwe na kupewa sifa ya ushujaa katika jamii. Kutompa heshima hiyo ni sawa na kumdharau na kuonesha kwamba kile anachofanya hakina mchango wala maana yoyote katika maendeleo ya taifa.

5.1.10 Mwanamke kama Mshauri katika jamii

Mwanamke amekuwa akisawiriwa kama mshauri wa jamii katika kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Tusomapo kazi za Penina Mhando kwa mfano tunakutana na mahali pengi ambapo mhusika bibi anatumika kama mshauri wa jamii. Kwa mfano katika tamthilia yake iitwayo Nguzo Mama kuna mhusika aitwae “Bi Msimulizi” ambaye kazi yake kubwa ni kutoa ushauri kwa jamii. Katika mashairi ya bongo fleva nayo mwanamke anasawiriwa vilivyo kama mshauri wa jamii pamoja na familia yake. Msanii Dudubaya katika wimbo wake wa *Mapenzi* anamsifu mpenzi wake kuwa ni mshauri mzuri pale anaposema:

Nakupenda mpenzi usiyependa *chapa*
Tikisa mshauri wa kweli
Wangu kimwana wangu we
Kimwali
Nadata na chako kiwiliwili
Kamwe hawategui kitendawili.

Katika dondoo hapo juu tunaoneshwa kuwa mwanamke ni mshauri mzuri sana wa familia yake pamoja na mume ama mchumba wake. Mshauri ni mtu anayetoa mawazo na maoni muafaka ya kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kwa jamii yake na taifa kwa ujumla. Katika msitari wa mwisho msanii anatumia sitiari kusema kwamba "kamwe hawategui kitendawili", kumaanisha kwamba, watu hawaelewi siri ya mafanikio yao katika familia yanatoka wapi. Kwa msingi huu maendeleo yao yanatokana na ushauri wa mwanamke kwa mume wake ndio unaowaongoza mpaka kupata maendeleo wanayoyapata.

Si hivyo tu bali pia ushauri anaoutoa mwanamke kwa mume wake ni ule wa kudumisha mapenzi yao ndiyo maana wanaishi kwa wema tangu waoane mpaka leo. Mawazo haya kimsingi yanapingana na yale aliyoyatoa msanii Lady Jaydee katika wimbo wake wa "wanaume kama mabinti." Katika wimbo huu mwanamke anasawiriwa kama kiumbe asiyekuwa na urazini wa kuweza kufikiri na kupanga masuala mbalimbali ya maendeleo yake yeye binafsi, familia yake na taifa kwa ujumla. Badala yake anamtegemea mwanaume kwa kila kitu. Hata hivyo, katika wimbo wa mpenzi tumeoneshwa kwamba mwanamke ni mshauri mzuri wa familia na jamii yake na anaweza kushauri juu ya mipango endelevu itakayoleta maendeleo kwa jamii na taifa kwa ujumla. Hata hivyo, tunachooneshwa hapa ni kwamba, huo ndio uhalisia wa maisha kwamba wapo wanawake ambao hawawezi kushauri vema

na wao huwategemea wanaume kwa kila jambo katika maisha yao. Vilevile, kwa upande wa pili wapo wanawake ambao ni washauri wa jamii na familia zao na ni wa bunifu na wapangaji wazuri wa mipango ya maendeleo. Hivyo haipendezi kutoa mtazamo wa moja kwa moja kwamba, mwanamke ni tegemezi na hana uwezo wa kutoa ushauri au kupanga mipango endelevu ya maendeleo katika jamii, bali yote mawili yanaweza kutokea.

Msanii Mwana FA katika wimbo wa *Hawajui* naye anazungumzia juu ya mwanamke kuwa ni mshauri wa mwenye mapenzi ya dhati. Anasema:

> “Umefunzwa utotoni umefundwa unyagoni kulea mwanaume lakini sio kama mimi asubuhi nilipoamka ukasema umeniota mimi. Una mapenzi hata shetani angeyaogopa sirudishi hata robo ya unavyonipa
>
> Hata washikaji zangu wanakiri kuwa sikufai kama ni adhabu nastahili nizikwe hai.

Katika wimbo huu msanii anatuonesha kwamba wapo wanawake ambao wana mapenzi ya dhati kwa wanaume wao lakini wanaume hawawajali wake zao hao. Msanii anatumia taswira ya unyagoni kutuonesha unyagoni kunatoa mafunzo mazuri katika kumlea na kumfunza mwanamke jinsi ya kumshauri na kutunza mume wake ili maisha yao yawe na amani na upendo kila siku iendayo kwa Mungu. Hata hivyo, shukurani ya punda ni mateke.

5.1.11 Mwanaume kama Kiumbe Msaliti wa Jamii

Kwa kuwa tunazungumzia usawiri wa masuala la kijinsia katika jamii ni dhahiri kwamba, tunazungumza juu ya wanawake na wanaume. Hivyo tunapozungumza juu ya usawiri wa mwanaume kama kiumbe msaliti kwa mkewe msomaji wetu

asishangae kwani ni kawaida kabisa kuyazungumza hapa. Tunasema hivi kwa sababu imezoeleka kwamba, masuala ya kijinsia huwahusu wanawake peke yao. Msanii Mwana FA anatuonesha namna mwanaume alivyokuwa kiumbe msaliti katika jamii. Anasema:

> Watoto wa nje kibao tena wasio na malezi
> Na matusi mama zao yote!
> Huja kwako
> Mpenzi nini unanipendea mwanaume
> Nina sifa mbaya rafiki zako wote wananiita
> Malaya napenda uwe na mume lakini sio
> Kama mimi sitaki tuachane nakuomba
> Uniache mimi hustahili uchezewe
> Sistahili kuwa na wewe umefanana na utulivu
> Kuwekwa ndani na uolewe.

Dondoo hili linatoa taswira kwamba mwanaume anajisema mwenyewe kuwa ni kiumbe msaliti pale ambapotoka nje ya ndoa yake na kuanza kufanya mapenzi na wanawake wengine ambao kwao huzaa watoto wa nje wasio na idadi. Mama wa watoto hawa, humtukana mke halali na mwanaume ambaye ni hawara yao lakini mama mvumilivu katulia tuli wala hana shida na mtu. Rafiki zake wanamtaka aachane na mwanaume huyu lakini yeye hawasikilizi na bado anaendelea kudunda na kumpenda mume wake licha ya usaliti wake.

Msanii anaendelea kueleza kwamba:

> Suruali zinanifunguka *vicheche*
> Vikikatisha mshahara ukitoka
> Sirudi mpaka umekwisha, nikirudi nae
> Usiku nalala na viatu, kicheche gani sikumbuki
> Hata ndoa yetu nikiwa na wewe moyoni napata aibu.”

Dondoo linaonesha kuwa mwanaume huyu ni msaliti wa ndoa yake pale ambapo anatembea na wanawake wa nje tena machangudoa. Inaelezwa bayana kwamba ni

kawaida yake kutembea na *vicheche* yaani wanawake malaya. Mbaya zaidi hata mshahara unapotoka wote huishia kwa wanawake hao wanaoitwa vicheche na mke wake huambulia mkia wa mbuzi. Mawazo haya kimsingi yanaonesha kwamba, suala la umalaya si la mwanamke peke yake kwani hata wanaume malaya nao wapo katika jamii na huu ndio ukweli kuhusu maisha. Kumsingizia mwanamke kuwa yeye ndiye malaya peke yake si sahihi na ni makosa makubwa. Watu wa aina hii wapo katika pande zote ukiwemo upande wa mwanamke na mwanaume.

5.2 Kufanana Kutofautiana kwa Wasanii wa Kike na Kiume katika Kusawiri Masuala ya Kijinsia

Katika utafiti huu tumepitia na kutumia mashairi ya bongo fleva ya wanawake na wanaume katika kusawiri masuala ya kijinsia katika jamii. Kuna kufanana na kutofuatiana baina ya wasanii wa kike na kiume wa nyimbo za bongo fleva katika kusawiri masuala ya kijinsia katika jamii. Msanii wa kike tuliyemtumia katika utafiti huu, Lady Jaydee anaonekana kumsawiri mwanamke katika mtazamo hasi na mwanaume katika mtazamo channya. Anamsawiri mwanamke kama kiumbe duni asiyeweza kupanga mipango endelevu ya maendeleo na badala yake anamtegemea mwanaume kwa kila kitu. Ameyasawiri haya kupitia kumlaani mwanamme anayetegemea kulishwa na ndugu zake au wazazi wake huku yeye binafsi hajitumi kwa kufanya kazi ili aweze kujitegemea. Kwa kufanya hivyo anamfananisha mwanaume huyu kuwa ni kama binti. Hii inashadidia hoja kwamba mwanamke ndiye anayestahili kulishwa na mwanaume ndiye mtafutaji wa maendeleo ambayo yatamnufaisha yeye binafsi pamoja na mwanamke.

Kwa upande wa wasanii wanaume ambao tumewatumia katika utafiti huu wanamsawiri mwanamke na mwanaume kwa mitazamo yote miwili yaani chanya na hasi. Kwa mfano, msanii Banana Zorro anamsawiri mwanamke kama mama na mlezi wa familia. Hakuishia hapo bali anaendelea kudai kwamba mama ni kiongozi wa familia na jamii katika maisha ya kila siku. Msanii Dudubaya kwa upande mwingine anamsawiri mwanamke kama mshauri wa familia na jamii kwa ujumla. Vilevile, anamsawiri mwanamke kama mtu mwenye mapenzi ya dhati kwa mume wake na familia yake. Hii ni tofauti na mawazo ya Lady Jaydee ambaye yeye anamtukuza sana mwanaume na kumshusha hadhi mwanamke kuwa ni tegemezi wa mwanaume kwa kila kitu.

Msanii Mwana FA kwa upande wake anamsawiri mwanaume kuwa ni kiumbe msaliti katika ndoa yake. Hii husababisha mwanaume huyu kuwa na watoto wa nje ambao hawapati malezi na matunzo stahiki ya baba na mama na kisha kuishia kuwa na watoto wa mtaani. Vilevile, mwanaume huyu ni malaya kwa sababu anatembea na wanawake wengi ambao humaliza mshahara wote wa mwanaume huyu na kushindwa kumudu mahitaji ya nyumbani kama vile chakula, mavazi na malazi. Kwa upande mwingine, mke wa bwana huyu ni mke mwema ambaye anampenda mume wake. Marafiki zake wanamshauri aachane na mwanaume huyu kutokana na tabia zake kuwa si za kuridhisha lakini yeye bado anampenda mwanamme huyo na kamwe hawezi kumuacha.

Kimsingi, kinachojitokeza katika mawazo ya Mwana FA ni kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe mvumilivu sana katika maisha ya kila siku. Waswahili

wanasema mvumilivu hula mbivu. Hii inamaanisha kwamba mwanamke huyu anavumilia na huenda siku moja mambo yakawa mazuri kwa mume wake kubadili tabia na kuwa mume mwema. Baada ya kubadili tabia wataishi maisha ya raha mustarehe kama mke na mume pamoja na familia yao.

Msanii Ferooz kwa upande wake anamsawiri mwanamke kama kiumbe dhaifu ambaye anaweza kudanganywa na wanaume na kufanya nao mapenzi bila kujiuliza juu ya madhara ya hali hiyo. Msanii anataja idadi kubwa ya wanawake ambao amefanya nao mapenzi kiasi kwamba amewasahau wengine kama alikwisha tembea nao na sasa anawataka tena kimwili. Hii inaonesha kwamba, mwanamke ni kiumbe ambaye ameumbwa kumstarehesha na kumburudisha mwanaume ndiyo maana huyu bwana akaweza kuwa ametembea na wanawake wote hao na hakuna hata mmoja aliyemkataa.

Si hivyo tu bali pia, msanii Ferooz anamsawiri mwanaume kama kiumbe mpenda starehe hasa starehe ya wanawake. Hii inaonekana pale mwanaume huyu anapokuwa ametembea na idadi kubwa ya wanawake ambao hata yeye mwenyewe hawakumbuki tena. Pia hii inamsawiri mwanaume kama kiumbe mwenye tamaa asiyeridhika hata kidogo. Ni tamaa tu ndizo zilizomfanya mwanaume huyu kutembea na idadi kubwa ya wanawake na si kitu kingine.

Kimsingi, katika sehemu hii tumeeleza kufanana na kutofautiana kwa wasanii wanawake na wanaume katika kusawiri masuala ya jinsia katika mashairi ya nyimbo za bongo fleva. Tumemuona msanii mwanamke Lad Jaydee akimsawiri mwanamke kwa mtazamo hasi na mwanaume kwa mtazamo chanya. Vilevile tumewaona

wasanii wa kiume kama vile Banana Zorro Dudubaya na Ferooz wakiwasawiri wanawake na wanaume katika mitazamo yote miwili; chanya na hasi. Hii inathibitisha ukweli wa maisha ambapo binadamu wapo wa aina mbalimbali na wenye pande tofauti tofauti. Wapo wale ambao ni wema na wengine ni waovu katika upande wa wanawake na wanaume pia. Hakuna jinsia iliyokamilika.

5.3 Mchango wa Tamathali za Usemi katika Kusukuma Mbele Masuala ya Kijinsia

Tamathali za usemi zina mchango mkubwa katika kusukuma mbele dhamira na maudhui mbalimbali yahusianayo na masuala ya jinsia katika mashairi ya nyimbo za bongo fleva. Kwanza, tamathali za usemi zimesaidia kujenga wahusika na matukio mbalimbali katika mashairi ya bongo fleva ili kusukuma mbele masuala ya kijinsia, kwa mfano, msanii mwana FA ametumia sitiari kama vile vicheche kuashiria wanawake wanaofanya shughuli ya ukahaba ili kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yao ya kila siku. Kupitia sitiari hii tunaweza kuelewa na kufafanua masuala mbalimbali ya kijinsia yanayoelezwa katika mashairi ya msanii huyu.

Naye Banana Zorro, ametumia sitiari mbalimbali kama vile *nguzo* na *taa* na kumpa mama sifa za vifaa hivyo. Sitiari hizi zimetusaidia kutambua kwamba, mama ni kiongozi, mlezi na mshauri wa familia katika maisha yao ya kila siku. Jengo bila nguzo haliwezi kusimama likatengamaa na watu wakaweza kuishi katika jengo hilo. Hivyo ni sawa na kusema kwamba, nyumba/familia bila mama haiwezi kutengamaa na kuitwa nyumba iliyokamilika kimalezi hasa kwa watoto na huduma kwa baba na wanajamii wengine. Msanii huyu pia anatueleza kwamba, mama ni *taa*, hii ina

maana kwamba mama ndiye muongoza njia ya maendeleo na mafanikio kwa familia yake.

Matumizi ya tashibiha mbalimbali nayo yametusaidia sana kuelewa maudhui mbalimbali yahusianayo na masuala ya kijinsia katika mashairi ya bongo fleva. Msanii Lady Jaydee anasema kwamba; wanakula na kunywa na kuvaa *wanaume kama mabinti*. Tashibiha wanaume kama mabinti inatueleza mambo mbalimbali yahusianayo na masuala ya kijinsia. Kwanza imetusaidia kuelewa kwamba, kumbe mwanamke ni kiumbe anayepaswa kuletewa kila kitu na mwanaume, hapaswi kutafuta maisha yake na kujitegemea kama ilivyo kwa mwanamke. Vilevile, tumeweza kuelewa kwamba mwanaume ni kiumbe shupavu ambaye anaweza kupanga juu ya maisha yake yeye mwenyewe na ya wale wanaomzunguka akiwemo mwanamke.

Msanii Prof Jay kupitia wimbo wake wa *Zali la Mentali* nae ametumia sitiari za aina mbalimbali kusawiri masuala ya kijinsia ili kuibua dhamira mbalimbali. Kwa mfano, anasema kwamba, alipotaka kuongea na binti mmoja ambaye alionekana kutoka katika tabaka la juu alijibiwa kwamba, “tafadhali we kinyago hii *ngoma ya gari*. Hii ni sitiari inayoonesha utabaka unaohusiana na masuala ya kijinsia katika jamii. Mwanaume masikini hawezi kuoa ama kuwa na urafiki na mwanamke tajiri na kinyume chake. Hata hivyo, msanii anaonesha kwamba, suala hili si la wanawake wote kwa kuwa wapo wanawake matajiri wanaowapenda wanaume masikini na kisha kuoana nao.

Kimsingi, zipo pia taswira na ishara mbalimbali ambazo watunzi wa mashairi ya bongo fleva wamezitumia katika kusawiri masuala mbalimbali yanayohusiana na jinsia. Kwa mfano, msanii Lady Jaydee anasema; “Kila upande wanafiki, wanaume kama mabinti”. Taswira inayopatikana hapa ni kwamba, mwanamke anasawiriwa kuwa ni mtu anayepoteza muda wake kwa kufanya mambo yasiyo na faida katika jamii na badala yake kuibomoa jamii kwa kuifikirisha. Kwa upande mwingine anatueleza kwamba, mwanaume hawezi kufanya mambo hayo kwani yeye anapaswa kufanya masuala ya maendeleo yatakayoliletea taifa maendeleo na si kufitinisha jamii kwa mambo yasiyo na msingi. Huu ndio machango wa taswira na ishara mbalimbali zilizotumiwa na msanii huyu katika kuibua dhamira na maudhui mbalimbali zinazohusiana na masuala ya jinsia katika jamii.

Wasanii wanaojulikana kwa jina la uswahilini matola kupitia wimbo wao *wa Kosa la Marehemu* wanatumia ishara katika kujenga masuala ya kijinsia. Kwa mfano, wanasema: *Kosa la Marehemu baba, sio kuvaa kondomu bali kuzini na mademu*. Tunachokipata hapa ni kwamba mwanamke anaonekana kuwa hana sauti katika masuala yanayohusiana na tendo la ndoa kwa maana kuwa anayepaswa kufanya maamuzi ya kuvaa kondomu au kutovaa ni mwanaume na si mwanamke. Ishara hii inaashiria mambo mengi kwa mfano hata katika maamuzi juu ya maisha ya familia ni mwanaume na si mwanamke. Mambo haya kwa pamoja yanachangia sana kurudisha nyuma maendeleo ya taifa kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, kwa kutovaa kondomu kunatokea maambukizi ya virusi vya UKIMWI na hivyo hupoteza nguvu kazi ya taifa. Pili, kutowashirikisha wanawake katika maamuzi ya familia na ujenzi

wa taifa kunasababisha kuunda mipango ambayo si imara na madhubuti katika kuliletea taifa maendeleo.

Matumizi ya tamathali za usemi ni nyenzo muafaka ya kimtindo inayotumiwa katika kumtofautisha mtunzi mmoja na mwingine. Kwa mfano utaona msanii Lady Jaydee hana matumizi mengi sana ya tamathali za usemi ukilinganisha na msanii Ferooz, Mwana FA na Prof Jay katika nyimbo zao. Matumizi ya tamathali za usemi kwa wingi yanamtaka msikilizaji kuzitafakari kwa undani zaidi tamathali za usemi zinazotumiwa na mwimbaji wa wimbo husika ili aweze kupata ujumbe uliokusudiwa na namna ilivyokusudiwa. Hata hivyo, wingi wa tamathali haina maana kuwa wimbo fulani unakuwa bora zaidi kuliko wimbo mwingine. Kwa mfano, wimbo wa Banana Zorro uitwao *Mama Yangu* unasitiari mbili kuu ambazo ni *Nguzo* na *taa* ambazo kwazo dhamira mbalimbali zimeweza kuibuliwa na kuufanya wimbo huu kuwa wimbo maarufu uliopendwa na wasikilizaji katika enzi zake.

Hivyo basi, tunaweza kueleza kwamba, tamathali za usemi zina mchango mkubwa katika kuibua na kueleza masuala ya kijinsia katika nyimbo za bongo fleva. Wasanii wa muziki huu kwa hakika wanatumia sana tamathali za usemi ambazo kwa ujumla zinaujenga muziki wao na kuwa muziki wa kizazi kipya kama unavyoitwa. Hata hivyo, matumizi ya tamathali hizo hayaufanyi muziki huu kupendwa tu na wanajamii bali pia huchangia katika kukuza msamiati wa lugha adhimu ya Kiswahili.

5.4 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Mjadala wa matokeo ya utafiti hufanywa ili kuweka bayana baadhi ya mambo ambayo mtafiti amekutana nayo na kuona ipo haja ya kuyafanyia mjadala ili pengine

yaweze kuibua utafiti zaidi. Miongoni mwa mambo ambayo yanahitaji kufanyiwa mjadala ni lile la msanii wa jinsia ya kike kumsawiri mwanamke kama kiumbe duni na asiyeweza kuwa mbunifu kama mwanaume katika kujiletea maendeleo na badala yake anakuwa ni mtu wa kufanya umbea na fitina katika jamii. Suala la kimjadala hapa ni kwamba, hivi ni kwa nini msanii mwanamke anamsawiri mwanamke mwenzake katika hali ya uhasi kama huo? Suala hili linahitajia mjadala zaidi.

Vilevile, katika utafiti huu tumeona kwamba, mwanamke anatajwa kuwa ni *nguzo* na *taa* imulikayo maisha ya jamii na familia katika kujenga nidhamu heshima na upendo kwa jamii. Suala la kimjadala hapa ni kwamba, hivi inawezekana mama peke yake bila msaada wa baba na wanajamii wengine akaweza kumlea mtoto mpaka akawa na maadili na nidhamu inayotakikana katika jamii? Suala hili linahitaji mjadala zaidi ili kupata suluhisho muafaka.

Pia katika uchambuzi wa data tumeona katika maeneo mbalimbali mwanamke akisawiriwa kama kiumbe mpenda starehe hasa zile zinazohusiana na masuala ya ngono ili aweze kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yake. Suala la kimjadala hapa ni kwamba, hivi ni kweli wanawake wafanyao ukabaha wote wanafanya ili kupata kipato cha kuwanufaisha wao peke yao au? Suala hili linahitaji kufanyiwa mjadala zaidi.

Vilevile, katika sehemu nyingi mwanaume naye anasawiriwa kama mchapakazi na kiongozi bora wa nyumba na familia. Tunayaona haya pale Lady Jay Dee anaposema kwamba, anamshangaa mwanaume anayetaka kulishwa na kuvishwa huku yeye binafsi hajishughulishi na kazi yoyote. Kwa kufanya hivyo anamfananisha

mwanaume huyo sawa na binti. Suala la kimjadala hapa ni kwamba, hivi ni sahihi kutumia kigezo alichotumia msanii katika kumfanisha mwanaume aliyemtaja na mwanamke? Suala hili nalo linahitaji mjadala zaidi.

Si hivyo, tu bali pia, suala jingine linalohitaji mjadala ni lile la kwamba, mwanamke naye apewe sifa ya ujasiri na ushujaa kutokana na shughuli mbalimbali anazofanya katika jamii. Kwanza kubeba mimba kwa muda wa miezi tisa na kisha kumlea mtoto mpaka aweze kujitegemea, kulea mume, ndugu wa mume na wake, kufua, kupika na kuosha vyombo. Kwa sababu hizi mwanamke anaweza kupewa sifa ya ushujaa kama ile apewayo mwanamme baada ya kushinda vita? Suala hili linahitaji kufanyiwa mjadala zaidi kabla ya kutolewa hitimisho la moja kwa moja.

Pia suala lingine linalohitaji mjadala zaidi ni lile la mwanamke tajiri kumpenda na kisha kuolewa na mwanaume masikini. Prof Jay anasema kwamba alipendwa na msichana aliyejulikana kwa jina la Vick ambaye anatoka katika familia ya kitajiri. Suala la kimjadala hapa ni kwamba hivi inawezekana ndoa ya mwanamke tajiri na mwanaume masikini ikadumu. Suala hili linahitaji mjadala zaidi na haitoshelezi kulitolea hitimisho la moja kwa moja katika muktadha huu.

Kimsingi, katika sehemu hii tumeeleza masuala mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa mjadala zaidi ambao unasaidia pia katika kuibua masuala mbalimbali ya kufanyiwa utafiti hapo baadaye. Mjadala wa matokeo ya utafiti unaonesha kwamba, masuala ya kijinsia ni nyeti na tata ambayo kamwe hayawezi kutolewa hitimisho la moja kwa moja. Kuyatolea hitimisho la moja kwa moja kutaonesha kupwaya kwa hitimishi hilo ndio maana nasi tukaamua kufungua milango kwa wanataaluma

kuyajadili na kuyachambua kwa kina. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kufika mahali tukakubaliana ama kupingana kwa hoja na kisha tukaweza kuikuza na kuiendeleza taaluma ya fasihi ya Kiswahili.

5.5 Hitimishi

Sura hii imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kwa minajili ya kujibu maswali yetu ya utafiti. Sura hii inaonesha kwamba nyimbo za bongo fleva zinaeleza masuala ya kijinsia kama yanavyojitokeza katika hali halisi ya maisha ya kila siku ya wanajamii. Kupitia tamathali mbalimbali za semi tumeweza kuona mwanamke na mwanaume wakisawiriwa kwa namna mbalimbali katika nyimbo hizo. Kwanza tumeona mwanamke akisawiriwa kama kiumbe tegemezi kwa mwanaume, mlezi wa familia, mshauri wa familia, jasiri na shupavu na kadhalika. Mwanaume naye amesawiriwa kama kiumbe mchapakazi, msaliti na kadhalika. Vilevile tumewalinganisha wasanii wanaume na wanawake katika usawiri wao wa masuala ya kijinsia na mwisho tukaonesha namna tamathali za usemi zilivyosaidia katika kuibua dhamira na maudhui mbalimbali katika nyimbo tulizoziteua.

SURA YA SITA

MUHUTASARI, HITIMISHI, NA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho katika tasinifu hii. Sura hii inawasilisha muhtasari hitimishi na mapendekezo ya utafiti wa baadaye. Muhtasari unafupisha yale ambayo yamewasilishwa katika kila sura wakati katika hitimishi matokeo ama mawazo makuu yaliyoibuka katika uchambuzi wa data yatatolewa na kuwasilishwa kama ipasavyo. Vile vile, katika mapendekezo; yatatolewa mapendekezo ya utafiti wa baadaye pamoja na masuala ya kisera.

6.2 Muhtasari

Utafiti huu una jumla ya sura Sita. Sura ya kwanza imeeleza kuhusu masuala ya kiutangulizi ambayo ndiyo yaliyotoa ithibati ya kufanyika kwa utafiti huu. Masuala hayo ni pamoja na mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, ambapo kuna lengo kuu na malengo mahususi pamoja na maswali ya utafiti. Vipengele vingine vilivyowasilishwa katika sura hii ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti. Vipengele vyote hivi ndivyo vimetoa ithibati ya kufanyika kwa utafiti huu.

Sura ya pili ya utafiti huu imefanya mapitio ya kazi tangulizi ambazo kimsingi ndizo zilizosaidia kubaini pengo la kiutafiti ambalo limeshughulikiwa na utafiti huu. Vipengele vilivyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na ufafanuzi wa istilahi kuu; tamathali za usemi zilizojumuisha tashibiha na tashihisi. Baada ya hapo tukawasilisha kipengele juu ya umuhimu wa istilahi tajwa katika kazi za fasihi na

utafiti wetu. Vipenge vingine vilivyowasilishwa katika sehemu hii ni tafiti tangulizi katika ushairi wa bongo fleva na matumizi ya tamathali za usemi katika kazi za fasihi kwa ujumla.

Sura ya tatu ya utafiti huu imewasilisha nadharia mbalimbali ambazo ndizo zilizo simamia uchambuzi wa data za utafiti huu. Nadharia zilizowasilishwa ni pamoja na nadharia ya Umarx, nadharia ya Simiotiki, na nadharia ya Ufeministi. Nadharia hizi kwa pamoja zimekuwa muhimili mkubwa katika kusukuma mbele utafiti wetu na kisha kukamilika.

Sura ya nne ya tasinifu hii imewasilisha mbinu na njia mbalimbali za utafiti ambazo zimetuongoza katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Njia na mbinu za utafiti zilizowasilishwa ni pamoja na usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa usampulishaji na sampuli. Vipengele vingine ni aina za sampuli; nasibu na madhumuni maalumu. Vipengele vingine ni mbinu za utafiti; mbinu ya usaili, usaili maalumu uliowazi. Mbinu ya majadiliano na kundi lengwa, na mbinu ya maktaba. Baada ya hapo zimewasilishwa zana za kukusanyia data kama vile matini, kompyuta na notibuku kinasa sauti, video kamera na kamera ya kawaida, na dodoso. Vilevile, tumewasilisha vipengele vya uhalali, kuaminika kwa data pamoja na maadili ya utafiti.

Sura ya tano ya utafiti huu imefanya uchambuzi wa data, matokeo pamoja na mjadala wa utafiti. Miongoni mwa mambo yaliyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na sifa za mwanamke dhidi ya mwanaume, mwanamke kama kiumbe anayedanganyika kirahisi, mwanamke kama chombo cha starehe, sifa na pambo kwa

mwanamke kupendwa na mwanaume, wanawake na mapenzi ya pesa na mwanamke kama mlezi wa jamii. Masuala mengine ni mama, kiumbe shujaa na jasiri. Mwanamke kama mshauri katika jamii na mwanaume kama kiumbe msaliti kwa jamii. Vilevile kufanana na kutofautiana kwa wasanii wa kike na kiume katika kujisawiri masala ya kijinsia na mchango wa tamathali za usemi katika kusukuma mbele masuala ya kijinsia navyo vimewasilishwa katika sura hii. Mambo haya yote kwa pamoja yamesaidia\ kukamilisha malengo ya utafiti wetu.

Sura ya sita ya tasinifu hii imewasilisha muhtasari, hitimishi na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

6.3 Hitimishi

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, mashairi ya bongo fleva yanahazina kubwa ya dhamira na maudhui yanayohusiana na masuala ya jinsia katika jamii. Mashairi haya yanaeleza masuala yanayowahusu wanawake na wanaume katika mahusiano yao ya maisha ya kila siku. Mtu yeyote ambaye si mtanzania lakini anapenda kufahamu masuala ya kijinsia katika jamii ya watanzania anaweza kuyapata masuala hayo katika mashairi ya bongo fleva. Kwa mfano, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, mwanamke anasawiriwa katika hali mbalimbali ambazo zinaonesha uhalisia wa maisha yake ya kila siku katika jamii. Anasawiriwa kama mama mlezi na mshauri wa jamii kwa upande mmoja. Kwa pande wa pili anasawiriwa kama msaliti, malaya, mzembe na mwenye mapenzi yasiyo ya dhati kwa mumewe.

Haikuishia hapo, mwanaume naye anasawiriwa katika picha mbalimbali kama vile, shujaa, jasiri, mchapakazi na mpenda maendeleo ya familia na taifa lake. Vilevile,

anasawiriwa kama msaliti, malaya, mlevi na mtelekeza watoto katika jamii. Haya yote kwa pamoja yanaonesha usawiri wa mwanamke na mwanaume ambao ndio uhalisia hasa wa maisha ya mwanadamu ulivyo. Wanadamu ana pande mbili yaani wema ama ubora na mapungufu yake.

Matokeo haya ya utafiti yanathibitisha nadharia kwamba fasihi ni zao la jamii na kamwe haiwezi kueleza mambo nje na jamii husika. Tunayasema haya kwa sababu hatukutegemea msanii wa kike kumsawiri mwanamke katika hali ya uhasi kama alivyofanya Lady Jaydee katika wimbo wake wa wanaume kama mabinti. Hata hivyo, kwa kuwa mfumo wa maisha uliopo bado unamtazama mwanamke kama kiumbe duni basi naye msanii kalazimika kufanya hivyo. Kwa mtazamo wake haoni kufanya hivyo ni kumdhalilisha ama kushusha hadhi ya mwanamke bali ni kawaida tu kwa kuwa mfumo uliopo ndio unaelekeza hivyo. Hata hivyo, masuala ya kumuona mwanamke kama kiumbe tegemezi yanakwenda yakiisha taratibu na jamii inawaona wanawake kuwa wanaweza na hawana tofauti yoyote na wanaume.

Hili linathibitishwa pale ambapo wasanii wanaume wanamsawiri mwanamke kama kiumbe jasiri na shujaa jambo ambalo katika miaka michache iliyopita halikupata kutokea. Sifa ya ushujaa ni sifa ya mwanaume peke yake huku mwanamke akibakia kutokuwa na sifa hiyo kabisa. Hata hivyo suala hili tumeliweka katika mjadala ili lijadiliwe zaidi ndipo hitimishi la jumla liweze kutolewa.

Vilevile, utafiti umebaini kwamba, wanaume na wanawake wanajiingiza katika vitendo vya umalaya kutokana na ulimbukeni usiokuwa na faida yoyote katika maisha yao dhidi ya kuwaongezea umasikini. Hii inadhihirika pale mtu mmoja

mwanaume anapoamua kutembea na wanawake kwa idadi kubwa kiasi kwamba, anashindwa kukumbuka ni wanawake wangapi aliotembea nao. Ulimbukeni huu ni ule wa kujidai kwamba ili aonekane kuwa yeye ni mwamba na mtu mashuhuri katika jamii yake basi anafanya hivyo bila kujali hata hatari ya kuaambukizwa magonjwa ya hatari kama vile UKIMWI. Hata hivyo, suala hili nalo tumeliweka katika mjadala ili tuweze kubaini sababu hasa zinazomsukuma mtu/mwanaume kutembea na idadi kubwa ya wanawake isiyohesabika kabla sisi hatujatoa hitimishi la jumla.

Vilevile, utafiti umebaini kwamba, mwanamke tajiri na mwanaume masikini wanaweza wakapendana na wakaishi pamoja. Hili limethibitishwa pale ambapo msichana tajiri alipompenda msukuma mkokoteni na kisha kufunga naye ndoa na kisha kuishi maisha ya kitajiri kwa pamoja. Vilevile, tumebaini kwamba, mwanaume masikini kwa upande mwingine amekuwa hapewi thamani na baadhi ya wanawake wanaopenda mali. Kutokana na mchango huu juu ya mwanamke tajiri kumkubali mwanaume masikini na mwanaume masikini kukataliwa na baadhi ya wanawake tukaona ni vema suala hili tuliweke katika mjadala ili lijadiliwe kwa kina zaidi kabla sisi hatujatoa hitimishi la moja kwa moja.

6.4 Mapendekezo

Kuhusiana na utafiti wa baadaye tunapendekeza kuwa, utafiti kama huu ufanyike katika kuchunguza namna tanzu nyingine za fasihi simulizi zinavyosawiri masuala ya kijinsia katika jamii.

Pia tunapendekeza utafiti wa kina ufanyike katika kuchunguza kukamilishana kwa vipengele mbalimbali vya tamathali za usemi katika kuibua maudhui na dhamira mbalimbali katika jamii.

MAREJELEO

Babbie, E (1992) *The Practice of Social Research*. 6th edition. Wadsworth Publishing Company.

Best, J.W. and Kahn, V. J. (2006). *Research in Education*. New York: Allyn Bacon Inc.

Barthes, R., (1994). *The Semiotic Challenge*. Berkely: University of California Press.

Furlong, N., na Lovelace, (2000). *Research Methods and Statistics*: *An Integrated Approach*. New York: Harcourt College Publis.

Chachage, S.L.C. (1991), *Alamasi za Bandia*, Dar es Salaam: DUP.

Chachage, S.L.C. (2000), *Makuadi wa Soko Huria*, Dar es Salaam: E and D Limited.

Cohen, L, Manion, L and Morrison, K (2000) *Research Methods in Education*. 5th edition. London: Rutledge Falmer.

Crewswell, J.W., (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications

Hussein, E., (1971). *Mashetani*. Oxford University Press: Nairobi

Hussein, E., (1976). *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Oxford University Press: Nairobi

Isaac and Michael, (1981). *Handbook of research and evolution*: *A collection of principles, methods and strategies useful in the planning, design and behavioural science*, San. Diago: Edips.

Jilala, H. (2008). The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania. MA Dissertation (Unpublished), University of Dar es Salaam.

Kahigi K.K. (1995). Lugha Katika Vitabu Vya Watoto. Katika *Kioo cha lugha: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (uk. 21-36).

Kezilahabi, E. (1971), *Rosa Mistika,* Nairobi: E.AL.B.

Kezilahabi, E., (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinnemen

Kezilahabi, E. (1990), *Nagona*, Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi E., (1991), *Mzingile*: DUP.

Kezilahabi E., (1999). *Kaptula la Marx*. Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi, E. (2008), *Dhifa*, Dar es Salaam: Videmuwa.

Kothari, C. K (1990) *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C.R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R (2001). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Ed. New Delhi: Wiley Eastern.

Kothari, R.C. (2004) *Research Methodology. Methods and Techniques* New Delhi: New Age International (P) Limited, Publishers.

Kothari, C. R (2008), *Research Methodology; Methods and Technique*, New Delhi: New Age International (P) Limited.

Kumar, R., (1999). *Research Methodology: A step-by-guide for beginners*. New Delhi: SAGE Publication

Lakoff, G. and Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. New York: Longman Group Inc. Limited.

Majembe, A.K. (1998), Language Use in Tanzanian Hip Hop Scene", Research Paper (Unpublished). Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Mangesho, P. (2003), "Global Cultural Trends: The Case of Hip Hop Music in Dar es Salaam". M.A Dissertation (Unpublished Dar es Salaam: Univesity of Dar es Salaam.

Momanyi. C. (2001). Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike na Uhakiki wa Kifasihi: *Kioo cha lugha.* Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Momanyi, C., (2007), Patriarchal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuated in Waswahili Poetry. The Journal of Pan African Studies, Vol.1, no. 8.

Msokile, M., (1993). *Uchambuzi na Uhakiki: Karibu Ndani,* Dar es Salaam: DUP.

Mulokozi, M. and Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH

Mutembei, A. (2009), UKIMWI katika fasihi ya Kiswahili 1982-2006. Dar es Salaam: TUKI.

Omari, S. (2009), "Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature", Unpublished Ph.D Dissertation, university of Dar es Salaam.

Omary, M. (2010) "Riwaya ya Kiswahili ya Majaribio: Uhakiki wa Ishara, Taswira, picha, sitiari na mafumbo zinavyoibua maudhui katika riwaya ya Nagona" Makala ya Semina: Haijachapishwa.

Omary, M., (2011), "Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008)", Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ogechi, N.O., Shittemi, N.I., Simala, K. I. (2008). Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.Moi University Press.

Robert, S. (1951), *Kusadikika*, London: Nelson

Robert, S. (1967), *Kufikirika*, Nairobi:OUP.

Robson, C., (2007). *How to do a research project: A guide for Undergraduate Students*, Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Senkoro, F.E.M.K., (1982). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP

Senkoro, F.E.M.K. (2003), "Rethinking Popular Arts and Culture in the 21st Century East Africa", Makala yaliyowasilishwa katika Maadhimisho ya 30 ya *CODERSRIA.*

Senkoro, F.E.M.K., (2006). "Fasihiya Kiswahili ya majaribio makutano baina ya Fasihi simulizi na Fasihi andishi", katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili chuo kikuu cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W., (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Yin, R. K., (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P.V., (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.

VIAMBATISHI

Kiambatisho Namba 1

Dodoso kwa ajili ya Wasanii wa Nyimbo za Bongo fleva

Utangulizi

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya Uzamili katika Kiswahili ninayesoma katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafafanya utafiti huu kama sharti pekee la kukamilisha utafiti wangu. Hivyo basi, ninaomba ushirikiano wako ili niweze kutimiza adhma hii muhimu katika taaluma ya Kiswahili.

Maswali

1. Naomba unitajie jina lako tafadhali
2. Eleza historia yako katika muziki wa Bongo fleva
3. Nitajie nyimbo ambazoumeimba mpaka sasa
4. Ni wimbo gani unaoupenda zaidi kuliko nyimbo nyingine?
5. Eleza sababu za kuupenda wimbo huo
6. Unaelewa nini kuhusu masuala ya kijinsia?
7. Eleza masuala ya kijinsia yanayojitokeza katika nyimbo zako
8. Kwa nini unamsawiri mwanamke hivyo unavyomsawiri?
9. Kwa nini unamsawiri mwanaume hivyo unavyomsawiri?
10. Eleza jambo lolote ambalo ni muhimu na mimi sijakuuliza

ASANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO

Kiambatisho Namba 2

Hojaji kwa ajili ya Hadhira ya Nyimbo za Bongo fleva

Utangulizi

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya Uzamili katika Kiswahili ninayesoma katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafafanya utafiti huu kama sharti pekee la kukamilisha utafiti wangu. Hivyo basi, ninaomba ushirikiano wako ili niweze kutimiza adhma hii muhimu katika taaluma ya Kiswahili.

Maswali

1. Naomba nitajie jina lako tafadhali……..
2. Nini mtazamo wako kuhusu historia ya nyimbo Bongo fleva

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……

   ……
3. Ni nyimbo zipi za wasanii wa Bongo fleva unazipenda zaidi?

   .....

   .....

   .....

   .....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

4. Kati ya Professa Jay, Lady Jaydee, Banana Zoro, Dudu Baya na Uswahilini Matola nani unayempenda zaidi?

.....

.....

.....

.....

5. Eleza sababu za kumpenda au kuwapenda wasanii uliowataja

……

……

……

……

……

6. Eleza masuala ya kijinsia yanayojitokeza katika nyimbo hizo

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

7. Kwa nini mwanamke anasawiriwa hivyo anavyosawiriwa katika nyimbo hizo?.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

8. Kwa nini mwanaume anaswiriwa hivyo katika nyimbo hizo?

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

9. Eleza jambo lolote ambalo ni muhimu katika utafiti huu name sijakuuliza……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

ASANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO